BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,018,116,895/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



## Anunua baiskeli kuwezesha usafiri wa mkewe kliniki

UKURASA 3



UKURASA 21

## LAPORTA AFUNGUKA HATIMA YA DE JONG

Jumapili Julai 31, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0581023
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Safu za uongozi CCM sasa pasua kichwa

**Viongozi** waifanya ajenda kila ziara, Kinana aonya watakaobainika...

*Endelea Uk. 2*

## Basi la wanafunzi lasimamishwa saa nane, polisi wabaini madudu

UKURASA 2



Askari kanzu (kushoto), akisimamia ubomoaji wa nyumba za wananchi wa eneo la Kimbesa Mpijimagohe, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana, ikidaiwa kuwa wamevamia eneo la mtu, ambapo zaidi ya nyumba 25 zimebomolewa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### BIL. 8/- ZATENGWA MRADI WA UMEME

SERIKALI imetoa Sh. bilioni nane kwa ajili ya kuanza kwa hatua za awali za ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa maji katika Mto Rumakali ulioko katika vijiji vya Madihani na Lumage, Makete mkoani Njombe...

UKURASA WA 4

### DK. MWINYI AONYA CHANGAMOTO ZA KIUSALAMA KWA MAENDELEO YA NCHI

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema changamoto za kiusalama katika taifa zinaweza kusababisha athari za kimaendeleo na ustawi wa mataifa mengine...

## Kamera kuwanasa wezi wa miundombinu ya barabara

UKURASA 3

MICHEZO **SIMBA SC, YANGA MPAKA KIELEWEKE** UK. 24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA




Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka (kushoto), akisoma moja ya mabango ya wananchi, baada ya Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Kanali mstaafu Abdulrahman Kinana (hayupo pichani), kutembelea stendi ya mabasi Katumba Azimio, Manispaa ya Sumbawanga, mkoani Rukwa, mapema wiki hii. **PICHA: CCM**

# Safu uongozi CCM pasua kichwa

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa** MBEYA

NI pasua kichwa. Ndivyo inavyoonekana kutokana na kila kiongozi wa ngazi ya juu ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) anaposimama akiwa katika ziara, anazungumzia suala la kuwapo makada wanaopanga safu za uongozi kwa ajili ya uchaguzi mkuu au wa ndani ya chama.

Hali hiyo inatokana na harakati za baadhi ya wanachama ama wanaowania nafasi za uongozi au wanaotaka kupata uongozi watakaowanufaisha baada ya uchaguzi. Kutokana na hali hiyo, inafanyika mipango ya chini kwa chini kuhakikisha azma ya kupanga safu zao inakamilika.

Baada ya viongozi kadhaa kuzungumzia hilo na kuwaonya watu wenye tabia hizo, Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Kanali Mstaafu Abdulrahman Kinana, naye ameibuka na kuzungumzia suala hilo.

Kutokana na kuwapo kwa mambo hayo, Kinana amewataka viongozi ndani ya chama hicho kuacha kujitengenezea safu katika uchaguzi wa ndani huku akiweka msimamo kuwa anayefanya hivyo hajiamini na hafai kuchaguliwa.

Kauli kama hiyo si ya mara ya kwanza kutolewa na viongozi wa CCM. Julai 13, mwaka huu, Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, alionya viongozi wa ndani ya chama hicho wanaokiuka kanuni na kupanga safu zao.

Chongolo alitoa kauli hiyo wakati akifungua mafunzo ya uongozi kwa viongozi wa mashina na matawi wa chama hicho na kusisitiza kuwa uchaguzi bado unaendelea na kinachomsikitisha ni watu kuutumia kupanga safu za uongozi zikiwamo ubunge na udiwani kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Mbali na Chongolo, Julai 8, mwaka huu, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) Itikadi na Uenezi Taifa, Shaka Hamdu Shaka, alizungumza na vyombo vya habari vya IPP Media baada ya kutembelea taasisi hizo. Alikiri kuwa changamoto za upangaji safu zipo na viongozi wa ngazi zote wamekuwa wakikemea.

Juzi, Kinana wakati akikamilisha ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo akiwasikiliza wanachama wa Mkoa wa Mbeya na kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya CCM, alionya wanaofanya hivyo.

Uamuzi huo aliufikia baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa mwanachama wakidai kuwa kuna baadhi ya viongozi wanapanga safu zao katika uchaguzi. "Onyo kutengeneza safu katika chama anayetengeneza safu yake katika chama hajiamini na hafai kuwa kiongozi, sasa unaona mtu anatengeneza safu kwa nini mnamchagua si mumpige chini.

"Lakini wapiga kura ndiyo nyie mnawajua kwa nini mnawachagua halafu mnakuja kusema ametengeneza safu, msiwachague hao wanaopanga safu bahati mbaya hujataja ni akina nani waliofanya hivyo umezungumzia jumla jumla ni marufuku watu kupanga safu zao za uongozi," alisema.

Kiongozi huyo alisema mtu mwingine ambaye hafai kwenye uchaguzi ni yule anayetoa rushwa kwa sababu ananunua cheo. "Akinunua cheo si chenu ni chake. Akishamaliza kuchaguliwa haonekani mpaka uchaguzi mwingine anajiona yeye ni mjanja atanunua tena cheo," alisema.

Kinana alisema rushwa ina pande mbili kwa anayepokea na anayetoa na kuwataka wanachama hao kumwomba Mungu awanusuru kuipokea rushwa.

"Kuna wengine ndio wataalamu wa kuuza kura. Anakwenda kwa mgombea anamwambia mambo kidogo ni magumu anataka umwambie sasa tunafanyaje. Inabidi umwambie tukae tuweke mikakati ya fedha. Akishapewa anakwenda kugawa asilimia 20 na asilimia 80 anabaki nazo," alisema.

Kuhusu malalamiko yanayotolewa kwa wataalamu wanaotekeleza miradi kudaiwa kutokuwa na ubora Kinana alisema wanaotakiwa kulaumiwa ni madiwani wanaowapa hizo kazi.

# Basi la wanafunzi lasimamishwa saa nane, polisi wabaini madudu

**Na Martha Sambo,** IRINGA

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Iringa, limezuia basi la Kimotco lililokuwa limebeba wanafunzi 62 baada ya kubainika ni bovu na halina mikanda.

Askari hao wa usalama barabarani, baada ya kulikamata basi hilo, walilisimamisha kwa saa nane kutokana na ukaguzi uliofanyika na kubaini madudu kadhaa jambo ambalo lilielezwa ilikuwa hatari kwa kusafirisha wanafunzi.

Hatua hiyo ya polisi imekuja ikiwa ni siku sita tangu kutokea ajali iliyoua watu 13 wakiwamo wanafunzi tisa mkoani Mtwara.

Basi hilo ambalo lilikuwa likiwasafirisha wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi ya Camaldoli wilayani Mufindi, linadaiwa kuanza safari saa 7:00 usiku kinyume cha sheria huku likiwa halijakaguliwa wala kupewa kibali cha kusafirisha wanafunzi.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Iringa, Mosi Ndozero, alisema ni kosa kisheria kwa basi lolote linalobeba wanafunzi kuanza safari usiku wa manane na bila kibali maalum cha kusafirisha abiria.

"Hii iwe ni onyo kwa mabasi mengine yote ni marufuku kupakia wanafunzi bila kibali na kukaguliwa, lakini pia sheria hairuhusu safari za usiku.

"Basi hili nalichukulia hatua za kisheria ili iwe fundisho. Mmeondoka usiku wa manane vipi kama lingetokea lolote?" alihoji.

Alisema baada ya basi hilo kutengenezwa kifaa kilichokuwa kimeharibika, ukaguzi ulibaini halina mikanda kwa ajili ya abiria na hivyo lilizuiliwa kuendelea na safari.

Mwalimu wa shule hiyo ambaye alikuwa mkuu wa msafara, Valence Ndembela, alikiri kuwa walianza safari usiku kwa shinikizo la wenye gari.

Alisema awali walikuwa wanawasiliana na wakala wa basi hilo aliyemtaja kwa jina moja Agrey ambaye aliwahakikishia kuwa ni zima na limefanyiwa ukaguzi.

Kwa upande wake, wakala wa basi hilo, aliyejitambulisha kwa jina la Agrey, alisema japo wanafunzi hao walipakiwa kwenye mabasi mengine mawili, mkoani Dodoma watarejeshwa kwenye gari lingine la kampuni yao lililokaguliwa.

Jumanne ya wiki hii, katika eneo la Mjimwema, Kata ya Magengeni, mkoani Mtwara kulitokea ajali iliyosababisha vifo vya watu 13 kati yao wanafunzi wakiwa tisa wa shule ya Msingi King David na kujeruhi 17.

# Kinyesi cha binadamu kutengeneza mkaa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

TOPE la kinyesi cha binadamu linatarajiwa kutumika kutengeneza mkaa kwa ajili ya matumizi ya kupikia hatua ambayo itasaidia kupunguza ukataji ovyo misitu kwa ajili ya nishati ya kuni na mkaa.

Hayo yalibainika juzi baada ya Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania, Wiebe de Boer, kuzindua mradi wa kutengeneza mkaa unaotokana na tope la kinyesi cha binadamu katika eneo la kuhifadhia taka kwa ajili ya urejelezaji, Muriet jijini hapa.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo, alisema mradi utakuwa na uwezo wa kuzalisha zaidi ya kilo 1,000 za mkaa kwa siku na utarahisisha upatikanaji wa nishati mbadala kwa wananchi.

Balozi huyo pia alisema mradi huo utapunguza kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira unaosababishwa na ukataji wa miti ovyo kwa ajili ya kuchoma mkaa kwa matumizi ya nyumbani.

Kadhalika, alisema mradi huo utaweka mazingira safi katika Jiji la Arusha na kutengeneza ajira kwa wananchi wa eneo hilo.

"Gari moja la kinyesi la mita za ujazo tano likimwagwa kwenye mazingira ni sawa na watu 500,000 kujisaidia ovyo bila ya kuwa na vyoo katika Jiji la Arusha. Kupitia Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira (AUWSA), kuna mpango wa kufikia asilimia 30 ya wakazi kuwa na mfumo wa maji taka na asilimia 70 wataendelea kutumia vyoo na huduma za kunyonya maji taka," alisema.

Pia alisema wametekeleza kwa pamoja mradi huo, kupitia makubaliano ya Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV), Jiji la Arusha na AUWSA.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, ambaye ni Ofisa Elimu wa Mkoa, Adam Mtupwa, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, John Mongella, alisema mradi huo ni mkubwa na utaleta manufaa kwa wananchi.

"Mradi huu ni mkubwa sana tunajiuliza swali je isingekuwa ufadhili wa wadau hawa kutoka Uholanzi sidhani kama ungeweza kutekelezwa kama ulivyokuwa sasa,"alisema.

Alisema serikali ya Tanzania inathamini na kutambua ushirikiano ulioko kati yake na nchi ya Uhalanzi hivyo aliahidi Mkoa huo utaendelea kushirikiana na kutunza mradi huo.

"Tunaahidi mradi huu utakuwa endelevu na hautakufa au kutetereka kwa kuwa kutakuwapo na usimamizi makini kutoka kwa watumishi wa serikali waliopewa jukumu hilo,"alisema.

Mkurugenzi wa SNV Tanzania, Michael Mcgrath, alisema mradi huo utasaidia kupunguza uharibifu wa mazingira hasa kwa kukata miti kwa ajili ya kupata nishati ya mkaa.

Mkurugenzi Mtendaji wa AUWSA, Juastine Rujomba, alisema jiji hilo lilipata mradi wa maji wa Sh. bilioni 520 ambao utakuwa na huduma ya maji safi na kuondoa maji taka katika eneo hilo.

## HABARI KITAIFA



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, wilayani Muheza, mkoani Tanga, wakijaza maji kwenye gari lao kwa kutumia ndoo baada ya yaliyokuwepo kuisha wakati wakizima moto uliozuka katika kiwanda cha mbao cha Prime Timber Ltd, kijiji cha Kwasemgaya, wilayani humo jana. Hakuna mtu aliyejeruhiwa katika tukio hilo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kamera kunasa wezi miundombinu ya barabara

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amesema mkakati endelevu wa kufunga kamera umewekwa ili kudhibiti wezi wa vyuma na minyororo iliyowekwa kwenye kingo za barabara.

Makalla aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam aliposhiriki usafi kwenye barabara za mkoa, kazi iliyohusisha wananchi na wakuu wa wilaya kila mmoja katika eneo lake.

Alisema mkakati wa uwekaji wa kamera utaanza na barabara inayotoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA) hadi katikati ya jiji.

Mkuu wa mkoa alisema serikali inatumia gharama nyingi kuweka kingo za barabara kwa kutumia vyuma na minyororo lakini baadhi ya wananchi wamekuwa waking'oa na kuviiba nyakati za usiku, hivyo kukosekana kwa ushahidi kwa aliyefanya kitendo hicho.

Alisema uwekaji wa kamera pia utahusisha soko la Kariakoo ili kuwezesha wafanyabiashara wake kufanya biashara zao kwa saa 24.

Kuhusu usafi wa mazingira, Makalla alisema wamepokea msaada wa vifaa mbalimbali vya usafi kutoka katika Kampuni ya Sigara ya Tanzania (TCC) ambayo imeunga mkono kampeni ya 'SAFISHA PENDEZESHA DAR ES SALAAM'.

Alisema TCC imetoa matoroli 50, mapipa 470 ya kuhifadhi taka, reki 50 na mafagio 50 na wameahidi kuendelea kutoa vifaa kila baada ya miezi miwili.

"Ninaipongeza na kuishukuru kampuni ya TCC Sigara kwa kushirikiana na Mkoa bega kwa bega kwenye Kampeni hii ya SAFISHA PENDEZESHA DAR ES SALAAM," alisema.

Makalla alisema katika awamu ya pili ya kampeni ya usafi mkoa umejipanga kuboresha na kupendezesha mandhari ya barabara kuu kwa kupanda miti, uwekaji bustani za watu kupumzika na mifumo ya umwagiliaji.

Pia alizitaka halmashauri kushirikiana na shirikisho la bodaboda kwenye ujenzi wa vituo vya kisasa vya bodaboda vilivyosajiliwa na kuratibiwa ili kupendezesha mandhari ya mkoa huo na kudhibiti uhalifu.

Mwenyekiti wa bodi wa Kampuni ya TCC Sigara, Paul Makanza, alisema wataendelea kushirikiana na mkuu wa mkoa kuhakikisha Dar es Salaam inakuwa safi.

# Bil. 8/- zatengwa mradi wa umeme

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI imetoa Sh. bilioni nane kwa ajili ya kuanza kwa hatua za awali za ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa maji katika Mto Rumakali ulioko katika vijiji vya Madihani na Lumage, Makete mkoani Njombe.

Akizungumza na wananchi wa vijiji hivyo jana, Waziri wa Nishati, January Makamba, alisema mradi huo unatarajiwa kuzalisha megawati 222 zitakazoingizwa katika gridi ya taifa ili kuongeza ufanisi wa mzunguko wa nishati ya umeme.

Waziri Makamba alisema mradi huo umesubiriwa kwa muda mrefu na ziara yake imelenga kuutazama na kutoa uhakika wa kuanza ujenzi wake.

Kuhusu suala la umeme vijijini Waziri Makamba alisema katika wilaya hiyo hakuna kijiji hata kimoja kitakachokosa.

"Ni kweli kulikuwa na matatizo ya kusuasua, baadhi ya maeneo yalikuwa kama yamesahaulika lakini tumesaini mikataba mipya na makandarasi wetu ambayo inahakikisha kila kijiji hapa Makete kinakuwa na umeme na kazi ya utekelezaji inaongezeka," alisema.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, Jasely Mwamwala alimweleza Waziri kuwa kuna haja ya kuongeza mkandarasi mwingine wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa sababu aliyepata kazi hiyo anazidiwa.

Mkandarasi anayetekeleza mradi wa umeme wa REA Mkoani humo, Mhandisi Nicholaus Lazaro, alikiri awali kulikuwa na matatizo lakini mchakato wa usambazaji umeme unaendelea na atahakikisha anatekeleza kwa mujibu wa mkataba wake.

# Anunua baiskeli kuwezesha usafiri wa mke wake kliniki

**Na Shaban Njia,** MBOGWE

KASHINDYE Kube (41), mkazi wa kijiji cha Mlale wilayani Mbogwe ambaye ni mnufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), amenunua baiskeli kutoka katika fedha anazopokea kuwezesha usafiri wa mke wake kwenda na kutoka kliniki ya ujauzito.

Kube amesema ameamua kufanya hivyo ikiwa ni sehemu ya kupambana na vifo vya wajawazito na watoto.

Aliyabainisha wiki hii alipotembelewa na maofisa wa TASAF kutoka makao makuu na wilayani waliofika kujua namna anavyotumia fedha zinazotolewa na mfuko huo na kunufaika nazo kwa kuzielekeza katika shughuli za ujasiriamali za kujiongezea kipato cha kaya.

Mnufaika huyo alisema kabla ya uwapo wa TASAF alikuwa akifanya vibarua katika mashamba ya watu na fedha alizozipata alikuwa akiendesha maisha na familia yake licha ya kuwa zilikuwa hazikidhi mahitaji na mwaka 2015 aliandikishwa kuwa miongoni mwa wanufaika wapya.

Alisema alianza kupata Sh.54,000 na kuzielekeza katika kilimo chenye tija kutokana na ushauri wa kulima kisasa kupitia maofisa ugani walioko kwenye kata yao na fedha alizozipata alinunua mbuzi, kuku na zingine alitumia kwa mahitaji ya wanafunzi.

Kube alisema baada ya mifugo kuongezeka na kuuza mbuzi 12, alipata Sh. 650,000 na kununua shamba lenye ukubwa wa ekari mbili jirani ya makazi yake na baiskeli ya kumpeleka mkewe na watoto kliniki kwa sababu bado wadogo na wanahitaji huduma.

"Mimi na mke wangu tunapopokea fedha za TASAF, tunakaa pamoja na kupanga nini cha kufanya chenye tija ndiyo maana mpaka sasa tumefanikiwa kupiga hatua katika maisha yetu. Sasa tuna shamba la ekari mbili tumelima mihogo," alisema Kube.

Alisema kutoka eneo analoishi hadi Zahanati ya kijiji ni umbali wa kilometa nne, kwenda Kituo cha Afya ni kilometa tano hali ambayo mkewe alikuwa akichukua muda mrefu kwenda kliniki badala ya kujikita kwenye uzalishaji mali hali iliyomfanya kuchukua kiasi cha fedha na kununua usafiri.

Pia alisema kwa sasa amelima mihogo na ana imani atapata mavuno mazuri na fedha atakazozipata atahakikisha anabadilisha maisha kwa kujenga nyumba ya kisasa na kuhakikisha watoto wake watatu kati ya saba, wanaosoma wanapata mahitaji yao yote ya shule.

Mke wa Kube, Lucia Nzumbi ambaye ndiyo mpokeaji wa fedha za TASAF, alisema wamefikia mafanikia hayo baada ya kuwapo kwa maelewano ndani ya familia kwa kupanga pamoja kwa kushirikisha na watoto baada ya kupokea fedha.

Hata hivyo, alisema wamejiunga vikundi mbalimbali vya ujasiriamali vilivyoko chini ya mpango wa kunusuru kaya masikini na wanaweka fedha na kukopeshana na kila mmoja amepewa mbuzi au ng'ombe na kuwahudumia na wanapouza wanagawana fedha na kuendesha maisha yao.


## TANZIA



***Mzee Gilead M. Tenga***

Mr. Freddy Gilead Tenga wa Arusha, anasikitika kutangaza kifo cha baba yake mzazi, **Mzee Gilead M. Tenga**, kilichotokea siku ya Alhamisi saa sita mchana ya tarehe **28.07.2022,** katika hospital ya Safi Medics, mjini Tanga.

Mipango ya maziko inafanyika nyumbani kwa marehemu, Bombo Area, Tanga.

Maziko yatafanyika katika makaburi ya Bombo Area, Tanga, siku ya ***Jumatatu tarehe 01.08.2022;*** baada ya ibada itakayofanyika nyumbani kwake mchana.

Habari ziwafikie Watoto wa marehemu Rose Gilead Tenga na Charles Gilead Tenga wakiwa Marekani, Robert Gilead Tenga akiwa Canada; wajukuu wa marehemu waliopo Marekani na Uingereza; Ukoo wote wa Ndorome Tenga; Ukoo wote wa Mmbaga; Familia ya Marehemu Mzee Said El Maamry; Ndugu, Jamaa na Marafiki popote walipo.

***BWANA alitoa, na BWANA ametwaa, Jina la BWANA na libarikiwe.***

***Amen.***

216971602

## Kampeni usafi mazingira yaja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema inatarajia kuanzisha kampeni kabambe ya kitaifa ya usafi wa mazingira ijulikanayo kama 'My Dustbin' ili kudhibiti utupaji wa taka ovyo kwenye mitaa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, aliyasema hayo jana jijini hapa aliposhiriki usafi katika soko la bonanza kwa kushirikiana na mabalozi wa mazingira Mkoa wa Dodoma.

Jafo alisema lengo la kampeni hiyo ni kuweka manispaa, miji na majiji kuwa katika hali ya usafi wakati wote.

"Kuna kampeni inakuja inaitwa 'My Dustbin'. Tunataka kila maeneo muwe mnaweka 'dustbin' (vifaa vya kuwekea taka) ili mtu akiwa na ganda la muwa anaweka au ndizi, chupa ya plastiki ili kujiepusha kutupa taka ovyo.

"Kampeni hii itakuwa nchi nzima na tutaizindua rasmi, lengo tunataka nchi yetu kila unapopita hukutani na karatasi wala takataka ya aina yoyote, na watu wa Jiji na Manispaa mtakuwa mnapita kukusanya na kupeleka dampo, lazima tutengeneze utamaduni wa usafi kwenye maisha yetu, nchi yetu lazima iwe kielelezo," alisema.

Waziri Jafo alionya yale maeneo ambayo yameanza kulegalega kwenye kufanya usafi na kuagiza wananchi wahakikishe wanaufanya. Pia aliagiza mikoa na halmashauri kutengeneza mikakati ya kuhakikisha masoko yaliyopo katika maeneo yao nayo yanakuwa safi.

"Miji na masoko mengi ni machafu kwa kuwa viongozi katika maeneo hayo hawaratibu vizuri ufanyaji usafi, ninaagiza kila mikoa na Halmashauri kutengeneza mikakati ya kuhakikisha masoko yanakuwa safi pamoja na kuratibu upatikanaji wa vifaa vya kuwekea taka ili kuweka mazingira kuwa safi," alisema.

Jafo alitumia fursa hiyo kuwapongeza mabalozi wa mazingira, wafanyabiashara soko la Bonanza na wananchi kwa kujitokeza kushiriki kufanya usafi na kuhimiza utaratibu huo uendelee ili kukabiliana na magonjwa ya mlipuko.

Katika hatua nyingine, Jafo alimtaka Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) ndani ya siku 14 kuhakikisha anaufanyia marekebisho mfumo wa maji taka katika soko hilo ili kuepuka uchafuzi wa mazingira.

Mkuu wa Idara ya Mazingira wa Jiji la Dodoma, Dickson Kimaro, alisema wameweka utaratibu wa ufanyaji usafi ili kuwa na mazingira safi.

Mwakilishi wa mabalozi wa mazingira, Emanuel Likuda, alisema wamekuwa wakihamasisha jamii katika kushiriki kutunza mazingira pamoja na kufanya usafi jijini humo.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, akiwa amebeba furushi la taka begani kupeleka dampo la soko la Bonanza, jijini Dodoma, aliposhiriki usafi ulioratibiwa na mabalozi wa mazingira wa sokoni hapo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dk. Mwinyi aonya changamoto za kiusalama kwa maendeleo ya nchi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema changamoto za kiusalama katika taifa zinaweza kusababisha athari za kimaendeleo na ustawi wa mataifa mengine.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana katika mahafali ya 10 ya Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC) kinachotoa mafunzo ya usalama na stratejia, yaliyofanyika Kunduchi, Dar es Salaam, akitolea mfano wa mgogoro katika ya Russia na Ukraine.

Alisema vita hivyo vimeathiri sana uchumi wa dunia kwa kusababisha pamoja na mambo mengine, ongezeko la bei za bidhaa, usalama wa chakula, uhamiaji, uhusiano wa kimataifa na kutetereka kwa hali ya kisiasa nje ya mataifa hayo.

Katika kukabiliana na changamoto zinazoikabili dunia hivi sasa, alisema itategemea namna Tanzania ilivyojitayarisha pamoja na uhusiano na mataifa mengine.

Kwa msingi huo, Rais Mwinyi alisema kuwa chuo hicho kinachofundisha masuala muhimu ya kiulinzi na kiusalama, kina umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya Tanzania na kwamba kuendelea kudumu kwa hali ya amani na utulivu ni msingi wa maendeleo ya taifa lolote lile.

Aliongeza kuwa ni dhahiri kwamba chuo hicho kinachofundisha mafunzo juu ya masuala muhimu ya kiulinzi na kiusalama, kina umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya nchi.

Chuo hicho, alisema ni muhimu hasa kwa wakati huu ambao dunia inakabiliwa na changamoto na matishio mengi ya kiulinzi na kiusalama vikiwamo vitendo vya kigaidi, vita na migogoro baina ya mataifa, vita vya wenyewe kwa wenyewe, wizi wa kimtandao, biashara na matumizi ya dawa za kulevya, uharibifu wa mazingira pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

Dk. Mwinyi alisema mafanikio ya kitaaluma ya chuo chochote kile yanategemea sana juhudi za chuo katika kufanya utafiti mbalimbali na kuweka mkazo wa matumizi ya tafiti hizo kwa maendeleo ya chuo na jamii kwa ujumla. Alisema kuna masuala muhimu ya ulinzi na usalama yanayohitaji kufanyiwa utafiti wa kina ili kuweza kukabiliana nayo, hivyo alisisitiza haja ya kuweka mkazo katika kufanya utafiti pamoja na kutumia na kusambaza matokeo ya utafiti kwa maendeleo na maslahi ya taifa.

Rais Dk. Mwinyi alisema ndani ya kipindi cha miaka 10, chuo hicho kimeendesha programu mbalimbali kwa viongozi wa ngazi za juu wa vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na wa taasisi zingine za serikali.

Alisema kuwa serikali zote mbili, ile ya Muungano na ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), zinapongeza na kufurahia kuona kwamba hivi sasa wako maofisa wengi ndani ya vyombo vya ulinzi na usalama na taasisi za serikali ambao wamepata mafunzo kutoka chuoni hapo na baadae kukabidhiwa nafasi nyeti na muhimu za uongozi.

Katika hatua nyingine, Dk. Mwinyi alipongeza uongozi na jumuiya ya chuo kwa kuendelea kufanya ziara za masomo za kwenda Zanzibar kila mwaka ikiwa ni sehemu ya mafunzo ya chuo hicho.

Alisema kwamba ziara hizo hutoa fursa ya kujifunza historia pamoja na kuona vivutio kadhaa vya utalii vilivyoko Zanzibar sambamba na kusikiliza uwasilishwaji wa mada zinazohusu masuala mbali mbali ya kisera, kiuchumi na kisiasa na kujionea hatua za utekelezaji wa mipango ya maendeleo ukiwemo uchumi wa bluu.

Mkuu wa Chuo cha Ulinzi wa Taifa (NDC), Meja Jenerali Ibrahim Mhona, alieleza mafanikio yaliyopatikana katika chuo hicho ambapo kwa mwaka huu wahitimu wake ni 43.

# Aweso aonya bei kandamizi za maji

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ameziagiza Bodi za Maji kuacha kuweka bei kandamizi kwa watumiaji wa huduma hiyo ili kuwawezesha kupata nguvu za kuendelea kutunza vyanzo vya maji.

Aweso alitoa agizo hilo jana mkoani hapa wakati akizindua mradi wa ujenzi wa ofisi na maabara ya kupima ubora wa maji pamoja na Bodi ya Sita ya Maji Bonde la Kati.

Waziri alitoa agizo hilo huku akisema baada ya kukamilika kwa mchakato wa Sensa ya Watu na Makazi, mabonde yote tisa ya maji nchini yarejee takwimu za upatikanaji wa maji nchini.

Aweso alizitaka bodi za maji kuhakikisha zinawatambua na kuwashirikisha watumiaji wa maji kwa kuwa wako baadhi wanayatumia bila vibali lakini hawatambuliwi.

"Moja ya matatizo ya mabonde yetu yanatumika tu kwa ajili ya kuvizia tu. Washirikisheni, watambueni wadau wenu wa maji na msiweke bei za kuwakandamiza, wekeni bei rafiki," aliagiza.

Aweso pia aliwataka wakurugenzi na maofisa wa mabonde ya maji kutambua wajibu wao kwa kutoka ofisini kutoa elimu sahihi ya namna ya uanzishwaji wa mabonde ya maji. "Wakati mwingine mtu anapoambiwa kuna taasisi ya bonde anajua pengine ni kimlima kidogo kidogo. Maofisa wa mabonde mtoke muwaelimishe wananchi," alisisitiza huku akisema haiwezekani mtu anajiita ofisa bonde halafu hata vyanzo vya maji havijui na wananchi wanapokuwa na matatizo, hakuna ufumbuzi.

Aliagiza zifanyike jitihada za kuongeza rasilimali za maji kwa sababu haiwezekani mvua zinanyesha halafu maji yote yanapotea kwenye bahari.

"Ni muda mwafaka rasilimali za maji kwa maana mvua zisiwe kama laana bali iwe baraka na fursa kwa maji yake kuvunwa kwa kujenga mabwawa ya kimkakati ili yatumike kwa matumizi ya kunywa," alisema.

Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji, Dk. George Lugomela, alisema Bodi ya Maji Bonde la Kati iliyomaliza muda wake imejitahidi kufanya kazi ambapo imeongeza ukusanyaji wa mapato kutoka Sh. milioni 300 zilizokuwa zikikusanywa awali na kufikia Sh. milioni 800.

## HABARI KITAIFA




Mkuu wa Oparesheni wa kampuni ya BayPort, Nderingo Materu (wa pili kushoto), akikabidhi nyaraka kwa Haji Manara, baada ya kutiliana saini makubaliano jijini Dar es Salaam juzi, ambapo Manara anakuwa Balozi wa kutangaza mikopo inayotolewa na kampuni hiyo, kwa ajili ya watumishi wa umma. Kulia ni Mkuu wa Mauzo wa kampuni hiyo, Lugano Kasambala na Mkuu wa Huduma kwa Wateja, Mercy Mgongolwa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Daktari ataka tahadhari homa ya mgunda

**Na Martha Sambo,** IRINGA

DAKTARI wa Mifugo wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Godbless Ngailo, ameitaka jamii kutumia nyama zilizokaguliwa na wataalamu wa mifugo ili kuepuka kukumbwa na homa ya mgunda

Akizungumza na Nipashe jana, daktari huyo alisema kwa mujibu wa utafiti uliotolewa, ugonjwa huo huenezwa na panya, hivyo watu wanatakiwa kujiepusha na matumizi ya kitoweo cha mnyama huyo.

Dk. Ngailo alisema ugonjwa wa Mgunda huambukiza kutoka kwa wanyama jamii ya panya, paka na wanyama wakubwa kama ng'ombe.

"Kimsingi ugonjwa huu kwa wanyama upo kwa kipindi kirefu na miongoni mwa wanyama ambao wamekuwa wakibeba vimelea vya ugonjwa huo ni paka, panya na ng'ombe," alisema.

Kutokana na ugonjwa huo kuwa tishio kwa afya ya binadamu, aliwataka watumiaji wa nyama kuhakikisha wanatumia nyama zilizothibitishwa na wataalamu wa mifugo ili kuchukua tahadhari kabla ya hatari. Pia aliwaondoa hofu kutohofia kula nyama zilizoko buchani kwa kile anachosema kuwa ni salama kwa kuwa zimepimwa na wataalamu kabla ya kuingizwa sokoni.

Alisema kuendelea kula nyama isiyokaguliwa na wataalamu wa mifugo ni kuhatarisha maisha.

"Kuna wengine wana tabia ya kula nyama ambazo hazijakaguliwa na wataalamu wa mifugo ni kuendelea kuhatarisha maisha yako na kwa wale wanaokula wanyama ambao hawajaidhinishwa kwa chakula kama panya ni kosa," alisema Dk. Ngailo.

Alisema panya ni benki ya bakteria wanaosababisha ugonjwa kama mgunda kwa binadamu.

Pia aliwataja wanyama wengine wanaoweza kuhatarisha maisha ya binadamu kwa kupata ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na wanyama wadogo wadogo wa kuwindwa kama sungura ambao hawajakaguliwa.

Baadhi ya watumiaji wa nyama, walisema tangu ugonjwa huo ubainike kusababisha madhara kwa binadamu, wamekosa imani na mboga hiyo wakihofia kupata madhara ya kiafya.

Elizabeth Sanga, mkazi wa Mkwawa Manispaa ya Iringa alisema iko haja ya serikali kufuatilia kwa ukaribu wafugaji wanaochinja mifugo yao nyumbani kiholela.

"Ulaji wa nyama umepungua kutokana na watu kuogopa ugonjwa wa mgunda ,kwa sababu watu wengi huchinja nyama kiholela majumbani. Tunaomba madaktari wafuatilie na kuwachukulia hatua wale wote wanaokiuka maagizo ya kitaalamu," alisema Elizabeth.

Hivi karibuni serikali ilisema homa ya Mgunda isiwe kikwazo kwa Watanzania kula nyama kwa kuwa asilimia kubwa ya nyama inayopitia machinjioni inakuwa salama.

## DIT, TGNP kuendeleza ubunifu, uvumbuzi

**Na Grace Gurisha**

TAASISI ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), imeingia makubaliano na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), kuanzisha na kuendesha programu ya pamoja ya kitovu cha teknolojia, jinsia na uvumbuzi. Akizungumza jana jijini Dar es Salaam baada ya kutia saini mkataba wa makubaliano hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, alisema utatekelezwa kwa miaka mitatu kwa lengo la kutengeneza uvumbuzi na ubunifu wa kiteknolojia ili kutatua matatizo ya kijinsia.

Liundi alisema lengo ni ili kurahisisha uwezeshaji wa wanawake na usawa wa kijinsia.

"Teknolojia imekuja na fursa nyingi za maendeleo lakini wanawake wengi hawayafikii maendeleo haya kutokana na sababu mbalimbali ndiyo maana tukaja na makubaliano haya," alisema.

Liundi alisema takwimu za mwaka 2019 za Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU) zinaonyesha kuwa kuna pengo la kijinsia kwa asilimia 10 katika matumizi ya mtandao duniani.

Alisema ukanda wa Jangwa la Sahara ni wa pili kwa kuwa na pengo kubwa la kijinsia kwa matumizi ya mtandao huo.

Kwa mujibu wa Liundi, kwa Tanzania takwimu hizo zinaonyesha kuwapo kwa pengo la kijinsia kwa asilimia 11 huku asilimia 77 ya watumiaji wa mtandao ni wanawake na asilimia 86 ni wanaume.

Alisema kutokana na takwimu hizo mafanikio ya wanaume yameweza kujulikana zaidi kuliko wanawake.

Mkuu wa DIT, Prof. Preksedis Ndomba alisema mchakato wa kuandaa bunifu hizo unawezekana kwa sababu taasisi hizo zote mbili malengo yake yanafanana. Alisema DIT ni taasisi inayotambulika ndani na nje ya Tanzania iliyobobea katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inayozingatia masuala ya jinsia katika taratibu zake ikiwamo aina ya kazi za kiteknolojia zinazotengenezwa na wanafunzi.

"DIT itaendelea kuwa kiongozi wa kutatua matatizo mbalimbali kwenye jamii kwa kutumia TEHAMA lengo ni kuendelea kutambulika Afrika na ulimwenguni," alisema Prof. Ndomba.

Alisema taasisi hiyo imebuni teknolojia nyingi ikiwemo atamizi ya mtoto njiti kumsaidia mtoto kupumua na mifumo ya kuweka taarifa ili kutatua matatizo yanayowakabili wananchi hususani waishio vijijini.

Ili kufikia usawa wa kijinsia, alisema DIT imeandaa mwongozo wa kuwashirikisha wanawake katika shughuli mbalimbali zinazofanywa chuoni hapa ili kukuza sayansi na teknolojia.

# Kamati yaundwa kubaini kero ardhi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Allan Kijazi, ameunda kamati kwa ajili ya kushughulikia migogoro ya ardhi mkoani Dar es Salaam.

Kutokana na kuundwa kwa kamati hiyo, amewataka wananchi wa mkoa huo kufika jengo la wizara, Magogoni kesho ili kutatuliwa kero na malalamiko yanayowakabili.

Dk. Kijazi alitoa wito huo kuwa wananchi wanapaswa kufika katika kambi itakayowekwa wizarani hapo kwa siku tano ili kusikiliza kero zao na kutatua baadhi ya zile ambazo zinaweza kupatiwa ufumbuzi.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imekuwa ikipokea malalamiko mengi ya migogoro ya ardhi, hasa inayohusu umiliki wa viwanja kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Arusha na Mbeya pamoja na jitihada za kutatua migogoro hii kwenye ngazi ya mikoa, na halmshauri zote.

Akizungumza na vyombo vya habari, Dk. Kijazi alisema wizara imebaini kwamba bado malalamiko ya wananchi yamekuwa mengi na mengine ya muda mrefu na kuwakatisha walalamikaji tamaa na katika maeneo mengine kumekuwa na hali ya kuzorota kwa amani.

"Hili ni suala ambalo tusingependa liendelee na kutokana na unyeti wa suala la ardhi, Uongozi wa Wizara umeamua kuweka nguvu ya kipekee kwenye kutatua kero ya migogoro ya ardhi kwa kuanzia na mikoa ambayo migogoro ni mingi," alisema.

Dk. Kijazi alisema ili kuboresha mifumo ya utendaji kazi kwenye wizara na kupunguza kero zisiendelee kujitokeza mara kwa mara, walalamikaji wanao uhuru wa kubainisha sababu za migogoro hiyo, ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Alisisitiza kuwa malalamiko yatakayofanyiwa kazi ni yale tu ambayo hayajawasilishwa mahakamani, kwa maana kwamba yasiwe kwenye mchakato wa usikilizwaji au yasiwe yameshatolewa uamuzi na mahakama.

"Kwa vile zoezi hili litagusa maeneo mengi ya nchi yetu, napenda pia kuwaarifu kwamba, pamoja na hatua ambazo Wizara inachukua kutatua malalamiko na kero za wananchi wa Dar es Salaam, tunaelewa kwamba jukumu letu la msingi ni kujenga utaratibu na mifumo ya kuzuia migogoro isijitokeze, na sio kusubiri migogoro ijitokeze ndio tuanze kuifanyia kazi," alisema.

Katibu Mkuu pia alisema malalamiko yatakayowasilishwa, kamati itakayasikiliza na kufanya uchambuzi wa kina kubaini sababu za malalamiko kuwa mengi, na kupendekeza hatua muafaka.

"Napenda pia kuwafahamisha kwamba, taarifa ya kamati ya kubaini sababu za malalamiko itakuwa sehemu ya hatua ambazo wizara imeanza kuchukua kufanya maboresho ya utaratibu na mifumo ya utoaji huduma ili kupunguza usumbufu na malalamiko ya wateja, ' alisema.

Dk. Kijazi alizitaja hatua zitakazochukuliwa kutatua migogoro ya ardhi kuwa ni kuwa na ofisi ya pamoja ya utoaji huduma kwa wananchi wanaohitaji huduma za ardhi kuanzia kesho.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ushauri wa Kinana kuhusu kodi unapaswa kuzingatiwa

**MAKAMU** Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana, wiki hii alifanya ziara ya kikazi katika mikoa ya Katavi, Rukwa, Songwe na Mbeya kwa ajili ya kukagua maendeleo ya chama pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi unaofanywa na taasisi mbalimbali zikiwamo mamlaka za serikali za mitaa.

Katika ziara hiyo aliyoambatana na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, Kinana alifanya mikutano ya hadhara na ya ndani kwa ajili ya kuzungumza na watendaji pamoja na kusikiliza kero za wananchi.

Miongoni mwa kero hizo ni pamoja na uwapo wa ututiri wa askari wa usalama barabarani ambao aliweka bayana kuwa wamekuwa kero kwa madereva na abiria kutokana na kusimamisha magari kila mara.

Hatua hiyo, Kinana alisema inafanya wananchi kushindwa kusafiri kwa amani huku akimwomba Mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, kuliangalia jambo hilo ikiwa ni pamaja na kuwapanga askari wa kikosi hicho kwa weledi ili watekeleze wajibu wao kwa ufasaha.

Licha ya jambo hilo ambalo jamii imelipokea kwa mtazamo chanya kutokana na kero hiyo kuwa sugu katika jamii, Kinana aligusia pia mfumo unaotumiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika kuwatoza kodi wafanyabiashara wadogo ambao alibainisha kuwa unawaumiza wananchi.

Katika kuelezea hilo, Kinana alisema mfumo wa kuwatoza wafanyabiashara wadogo wakiwamo wale wanaoanza ujasiriamali, ni kandamizi na unapaswa kuangaliwa upya ili kutengeneza mazingira rafiki kwa walipakodi na kuleta maendeleo endelevu kwa uchumi wa taifa.

Makamu mwenyekiti huyo alitoa mfano wa mtu anayeanza biashara kwamba kabla ya kufanya chochote, anatakiwa kufanyiwa makadirio ya kodi ambayo sehemu yake anapaswa kulipa kabla ya kuanza. Kwa maana hiyo, mjasiriamali huyo anapaswa kulipa kodi hata kabla ya kuanza biashara.


Kinana alisema kwa mantiki hiyo, mtu huyo kama ana mtaji wa Sh. Milioni moja, anapaswa kulipa kodi kwa kutumia sehemu ya mtaji huo, jambo ambalo linachangia kumdidimiza badala ya kupiga hatua. Matokeo yake, ni ngumu kwa mfanyabiashara huyo kukuza biashara yake.

Ni vyema TRA ikapokea ushauri huo wa Kinana na kuufanyia kazi ili kuleta mageuzi ya kiuchumi kwa kuwezesha wafanyabiashara wadogo kupata kukua kimtaji na hatimaye kuwa na ukwasi ambao kwa kiwango kikubwa utawawezesha kulipa kodi ambayo itatumika katika miradi ya maendeleo.

Kama alivyosema mwasisi wa taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, hakuna nchi duniani inayoweza kupiga hatua kimaendeleo kama haikusanyi kodi, ni dhahiri kwamba kodi ni muhimu lakini kunapaswa kuwa na mazingira rafiki kwa wafanyabiashara.

Kwa mantiki hiyo, TRA kama alivyoshauri Kinana, inapaswa kwanza kuwatambua na kuwasajili wajasiriamali na kuweka mazingira ambayo yatawafanya wajisikie vizuri baada ya kupewa muda fulani wa kufanya biashara kabla ya kuanza kulipa kodi kama ilivyo sasa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Ugonjwa wa UVIKO-19 bado upo, tusijisahau

**INAONEKANA** kana kwamba ugonjwa wa UVIKO-19 umeisha kutokana na jinsi mambo yanavyoendelea kwa sasa, hata zile sehemu ambazo zilikuwa na vitakasa mikono na kulazimishwa kuvaa barakoa, hakuna tena.

Sehemu ambayo inaonekana bado inahitaji watu kuvaa barakoa ni hospitali pekee wakati sehemu nyingi zilizobaki maisha yamerudi kama kawaida. Si sehemu za serikali, watu binafsi, au kwenye mikusanyiko mingine kama vituo vya mabasi, treni, au za burudani, kumeanza uzembe wa kutokuwa na maji ya kunawa, sabuni au vitakasa mikono.

Kwa maana hiyo, wananchi wengi wameendelea na maisha yao yale yale ya mwanzo ya kudhani kuwa ugonjwa huo umemalizika.

Ukweli ni kwamba ugonjwa huo bado upo na unaendelea kugharimu maisha ya wapendwa wetu kama ilivyokuwa mwanzo, licha ya kwamba kwa sasa maambukizo ni madogo tofauti na mwanzo kutokana na elimu kubwa kutolewa, pamoja na jitihada za serikali.

Pamoja na hayo, hata ile idadi ndogo wa wagonjwa au wanaopoteza maisha haifai kukaliwa kimya kwa sababu bado ni wapendwa wetu.

Tanzania ni nchi pekee Afrika Mashariki ambayo ilikabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19 kwa namna ya pekee ambayo imekuwa mfano wa kuigwa, kiasi cha kuanza kufanyiwa kazi na mataifa mengine. Haikuzuia wananchi wake majumbani, badala yake ikawaambia waendelee na shughuli zao kama kawaida za kujipatia kipato cha kila siku, lakini ikawatahadharisha kuwa makini kwa kuchukua tahadhari ya ugonjwa huo.

Ikawambia wananchi wake nini cha kufanya wanapotoka nyumbani, kusalimiana, jinsi ya kupanda kwenye vyombo vya usafiri vya umma, na hata wanapokuwa kwenye sehemu zao za kazi.

Wakati huo nchi nyingi ziliwafungia wananchi wao ndani, kiasi kwamba kulileta matatizo mengi kuliko athari ya ugonjwa wenyewe, ikiwemo kuporomoka kwa uchumi kwenye nchi hizo.

Wananchi wa nchi jirani wakaanza kuzilalamikia serikali zao na kuwaambia waige mfano wa Tanzania. Taratibu wakaanza kuwaruhusu na kuiga jinsi Tanzania ilivyolichukulia suala hilo na kulifanyia kazi kwa namna ya pekee.

Kama nilivyosema mwanzo, ni kweli maambukizi kwa sasa si mengi kwa sababu baadhi ya wananchi wamepata chanjo na wengine wanaendelea kupata, hata hivyo waliobaki wanaona ni kama vile mambo yameisha.

Hilo limemsukuma Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu kutoa tahadhari ya ugonjwa huo, ukiwemo pia ugonjwa mwingine wa Mgunda uliogundulika Julai 18 mwaka huu.

Waziri alisema hatuna budi kujikinga na ugonjwa huu ikiwamo kuvaa barakoa hasa tukiwa ndani kama hapa tulitakiwa kuvaa barakoa kwa sababu wengi hamjachanja, tuhakikishe tunanawa mikono mara kwa mara.

Pamoja na hayo, aliwataka Waganga Wakuu wa Mikoa kuhakikisha sehemu zote za umma kunakuwa na vifaa vya kunawia mikono, maji tiririka pamoja na sabuni au vitakasa mikono. Tunataka vifaa hivyo virudi tena katika ofisi zetu kwa ajili ya kujikinga na magonjwa ya kuambukiza ukiwemo ugonjwa wa kipindupindu na kuhara damu.

Wakati anasema hayo, ina maana watu wengi walikuwa hawajavaa barakoa, na hii yote ni kuonyesha kuwa wananchi wameanza kupuuzia na kuona kama umekwisha.

Waziri akasisitiza wananchi waendelee kujitokeza kuchanja kwa sababu mwamko unaonekana ni mzuri.

Pia alibainisha kuwa asilimia 99 ya watu wote wanaougua ugonjwa huo na kulazwa hospitalini ni wale ambao hawajachanja.

Hapa inaonyesha kuwa wanaochanja wanakuwa wametengeneza kinga kiasi kwamba wengi sasa hawapati tena maambukizo hayo, badala yake unawapata ambao mpaka sasa hawataki, au wanachukua muda mrefu kujishauri kwenda kuchanja.

Huu sasa uwe wito kwa wananchi kwanza kujua kuwa bado ugonjwa huo upo na unaendelea kuwapata kwa asilimia kubwa wale ambao hawajachanja.

Cha muhimu hapa ni kwenda kupata chanjo. Lakini pia iwe kwa waliochanja au wasiochanja wasijiachie sana, badala yake wanatakiwa waendelee kuwa na tahadhari kuhakikisha hawapati maambukizo hayo au hawawaambukizi wengine, ili nchi isirudi kule ilikotoka.

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Hatimaye nimeupata uwakili, Je, nitakuwa kama Lakha?- 3



Na Pascal Mayalla

KATIKA mwendelezo wa makala hii, tangu mwanzo nilieleza kuwa nilitamani kuwa wakili kwa sababu ya Wakili Murthaza Lakha toka mwaka 1976. Hatimaye sasa nimekuwa wakili lakini swali la kujiuliza, je, nitakuwa kama Lakha?

Wiki iliyopita, tuliishia Baba Mzee Andrew Mayalla kuwa ni miongoni mwa washtakiwa wa kesi ya mauaji Mwanza, iliyowang'oa madarakani kuanzia Makamu wa Pili wa Rais, Mzee Rashidi Mfaume Kawawa, mawaziri wawili, mkuu wa mkoa na maofisa waandamizi wa serikali mkoani Mwanza kutokana na vifo vya watuhumiwa wawili, Masaga Mahula Mazengenuka na Isaack Ngw'ana Nkog'oboko waliokufa mikononi mwa polisi muda mfupi baada ya mahojiano.

Kwenye utekelezaji wa baadhi ya mambo ya baadhi ya idara za serikali, kuna watu wema, wanaolazimika kufanya maovu katika kutekeleza wajibu wao lakini dhamira zao ndizo zinazowasuta.

Vikao kazi ndivyo vilivyoamua ni mbinu gani zitatumika kuwahoji watuhumiwa, naomba nisizitaje humu, lakini kosa la Mzee Mayalla ni huruma ilimponza.

Baada ya watuhumiwa hao kuhojiwa, Mzee Mayalla akaingia huruma, kumbe kwenye mkoa, Kamanda wa Polisi wa Mkoa (RPC) yuko chini ya Ofisa Usalama wa Mkoa (RSO), hivyo Mzee akaamuru mahojiano ya wawili hao yasimame. Kutokana na alivyowaona akaamua kujitolea kuwabeba kwenye gari lake kwenda kuwakabidhi hospitalini wapatiwe matibabu, kumbe wema unaponza.

Wakati wakiwa njiani ndipo wakamweleza mzee kuwa hawajala siku nne! Mzee akaamua kusimama njiani wapate chochote, wakawa hawawezi kutembea! Wakaagiziwa soda na keki wakaletewa hapo hapo kwenye gari, ile kunywa tuu, kidogo, walitapika damu na kuzimia, hivyo akawakimbiza Bugando.

Kule kwanza walikataliwa kupokewa mpaka polisi watoe PF 4! Polisi wakagoma kwa hoja kuwa ofisa huyo amewaiba mahabusu na kuwasafirisha kwa gari binafsi bila utaratibu, hivyo chochote kikitokea hawatahusika.

Akampigia daktari mkuu wa Bugando, wakati huo Dk. Nkulila, akatoa amri wapokewe na wakapokewa nakupatiwa huduma ya kwanza.

Mzee akarudi nyumbani. Kesho yake asubuhi ilikuwa natoka na baba na kuniacha kwanza shuleni ndipo aende kazini. Mimi nilikuwa wa kwanza kuingia kwenye gari, siku hiyo nikakuta kiti cha nyuma kimetapakaa damu! Nilikuwa nakalishwa nyuma hata kama mbele hakuna mtu.

Kumbe wale watuhumiwa wote wawili, kufika asubuhi walikuwa wamepoteza maisha!

Mzee akageuziwa kibao. Kwa kifupi, Mzee aliamua kusema ukweli wote juu ya kilichotokea. Mwisho wa siku kati ya washtakiwa wote, ni Mzee Mayalla pekee alikutwa hana hatia na kuachiwa, watuhumiwa wengine wote walifungwa vifungo virefu.

Hili liliwezekana kwa sababu tu ya umahiri na utetezi wa Wakili Murtaza Lakha. Ndipo mimi nikaamua nikiwa mkubwa lazima niwe wakili ili nitetee wanaonewa.

Maisha ya Mzee baada ya kesi hiyo, hayakuwa kama awali asilani. Kitu ambacho aliendelea kuwa nacho ni jicho la kuangazia warembo.

Nakumbuka siku moja Jumapili, tukiwa wote kwa Mzee Kasanga, kuna jirani yetu mmoja ni chotara akiitwa Stefa. Mzee kumwona Stefa, akaninyooshea ishara ya dole gumba kuwa unajua kuchagua!. Kumbe mimi na Stefa hatukuwa na jambo lolote zaidi ya kuwa marafiki tu. Baadaye aliniuliza Yule ndiye mkamwana? Nikamwambia hapana, kwa nini?

Wakati Baba akiwa kwenye kesi kule Tabora, Mzee Kasanga pia alimhamisha bibi akaja Dar es Salaam na mimi kuianza safari rasmi ya kuutafuta uwakili, hivyo wote tukawa Dar es Salaam. Nyumba ya Drive In ikawa haitoshi, Mzee Mayalla akakaa kwa baba yangu mkubwa Mzee Mfaume, Magomeni Mapipa, baadaye akapata kazi kama ofisa usalama mkuu wa kampuni ya Wataliano ya Cogiffer na kuhamia Zanzibar.

Katika Shule ya Sekondari Tambaza tulisoma masomo yote hadi kidato cha pili na badaaye nikaingia katika mchepuo wa masomo ya sanaa. Kulikuwa na mwalimu wetu mmoja shuleni pale jirani yetu Drive In, akaja kunishitaki nyumbani kuwa mtoto ana akili, lakini amechagua fani ya majinga!. Nikaitwa na Mzee Kasanga mbele ya mwalimu na kuulizwa kwa nini nimechagua masomo ya wajinga, nikajibu nataka kuwa kama Lakha!.

Niligomewa, Mwalimu Kalunga akaambiwa nirudishwe masomo ya sayansi, lakini niliamua kusoma yote yaani sayansi na yale ya sanaa.

Matokeo ya kidato cha nne yalipotoka nilipata A moja ya siasa, B ya Kiingereza na kutandika makarai yote kwa masomo yaliyobakia, hivyo nikapangiwa kwenda kusoma Historia, Jiografia na Kiingereza (HGL) Ilboru, Arusha.

Baada ya kujiunga na Shule ya Sekondari ya Ilboru, kutokana na kuambiwa nilipokuwa Tambaza kwamba ili usome sheria ni lazima upate daraja la kwanza kidato cha sita.

Kwa hiyo niliamua kupambana ili nipate matokeo hayo lakini haikuwa hivyo na ndoto ya uwakili na kuwa kama Lakha ikakatikia hapo.

Hata hivyo kwa sasa nimekuwa wakili. Funzo la simulizi hii ni kwamba kuna vitu unaweza kuvipanga lakini kama Mungu hajakupangia haviwi. Lakini kama Mungu amekupangia, vinaweza kutimia hata ukiwa na miaka 80 kama mke wa Ibrahim alipomzaa Isaka.

**Wasalaam**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Matrafiki wakumbushwe wajibu, wapangwe tu!



Na Joseph Kulangwa

**Majaliwa wa Majaliwa keshamaliza mchezo. Kimeeleweka na sasa tusonge tu mbele na kazi iendelee. Unajua wakati mwingine tuwe tunaangalia na uchumi unakwendaje, hivi hamkuona Uviko-19 ulivyotusambaratisha? Mnajifanya hamjui kuwa Putin na Zelensky wanafanya yao huko mpaka sisi huku maji tunaita mma?**

NI mwisho wa mwezi, namsaka jamaa yangu anayefanya kazi huko ummani aliyeniahidi kuwa baada ya nyongeza ya mishahara atanitafuta kunionyesha jeuri yake.

Sijamwona mpaka sasa na hata kwa simu simpati sijui ni kwa nini. Nadhani anagugumia alichokisubiri anitambie mimi wa ubinafsini huku, lakini hakukiona!

Mi nilimwambia mla ni mla leo mla jana hajala kitu, hakuniamini mpaka alipomsikia Mheshimwa Majaliwa wa Majaliwa akimwambia ile nyongeza ilikuwa ya wale wa kima cha chini, Nadhani ndiyo sababu kaamua kunifungia vioo.

Hajui kuwa mimi huwa sijali na nasubiri zamu yangu kwani wakubwa bado wanatujadili nasi tuongezwe kiasi gani, asilimia 23.3 kama wenzetu au vipi. Najua tena huku kwetu ubinafsini huwa kuna mizengwe ile mbaya.

Huku mnaweza mkakaa bila kulipwa hata hiyo mishahara ya zamani kwa miezi kadhaa lakini msishituke kwani kuna mitikasi mingi ya kumpiga tajiri changa la macho na maisha yakasonga.

Hata msipotukumbuka sisi, aah wapi, tutakula humu humu kwenye malori ya ubinafsini na mkileta za kuleta tunayaweka kandoni mwa barabara au tunayalambisha vumbi au kuyakalisha kwenye mawe.

Lakini inshalah, wenzetu wa ummani tayari wameshajua mwelekeo wao, Majaliwa wa Majaliwa keshamaliza mchezo. Kimeeleweka na sasa tusonge tu mbele na kazi iendelee.

Unajua wakati mwingine tuwe tunaangalia na uchumi unakwendaje, hivi hamkuona Uviko-19 ulivyotusambaratisha? Mnajifanya hamjui kuwa Putin na Zelensky wanafanya yao huko mpaka sisi huku maji tunaita mma?

Hebu tujifunze kuvumilia bhana, mbona tulikaa miaka saba hakuna aliyepanua domo kuulizia na kusema? Tumsaidie Chifu Hangaya aendelee kupambana, aendelee kukopa nje, tuletewe za Uviko zingine tujengee miundombinu na mambo mengine ya nchi, tubuni tena Royo Tua lingine, waje watuletee midola tuhangaike nayo.

Jamani hizo zilikuwa tu salamu zangu. Hoja yangu ya leo ni hii ya Kanali mstaafu Abdul Kinana, ya kutaka jamaa zetu matrafiki kupungua mitaa ya mijini, ili angalau wenye mandinga yao wapumue.

Ila kwa kweli sisi madereva kazi tunaipata humo barabarani tunapoona magwanda meupe tu kwa mbali, unajua usiposimamishwa basi utakuwa hujaonwa au umeamka vizuri, sasa sijui ni uraibu wa kusimamisha magari au nini!

Kwa kweli adha hiyo ipo sana katika miji yetu hii, lakini tunajua nini sababu yake. Ndivyo maisha yalivyo kama ambavyo sisi wa ubinafsini, tunavyowakomesha matajiri zetu, nadhani ndivyo hata jamaa hawa wanatukomesha.

Mi naunga mkono hoja ya Kinana lakini sikubaliani nayo asilimia zote kwa sababu hawa jamaa kwanza si wengi kihivyo. Bahati mbaya hupenda tu kukaa pamoja na ndiyo sababu wanakuwa wengi.

Mijini kuna magari mengi, hivyo bila wao kuwapo au kuwa wachache, walahi nakwambieni itatokea zahama ya kuua mtu, ambapo kutakuwa na mingarangara iliyofia barabarani na isikalishwe pembeni na tutajua nini maana ya foleni.

Sikatai, kwamba baadhi yao, si wote, wamekumbwa na uraibu wa kuona kila gari likipita basi lina makosa, na wengine wakisimamisha wanakuwa hawana la kusema zaidi ya kuuliza maswali mwingine hata hayahusu gari ili mradi ukasirike utafutiwe la kutafutwa.

Wengine bila kutafuna maneno, wanalazimisha kupata kitu kidogo ili uachwe hata kama huna makosa. Hiyo nayo ni kero kwa kweli.

Ila kuwapunguza mijini wahamie kwingine kusiko magari mengi ni kutaka kuwapumzisha tu na wengine wanaweza kuacha hata kazi kwa sababu watakuwa hawapati 'kazi' ati!

Mkisema muwaondoe, mjue ajali zitakuondoeni haraka sana. Wanapokuwapo na kukusimamisheni wanasaidia sana kuwaepusha na mauti. Kinachotakiwa ni kuwapa elimu tu, wakumbuke au kujua misingi ya kazi yao, kwamba si kuonea, si kusimamisha magari kwa sababu ya kusimamisha tu, bali kuhakikisha usalama.

Mambo mengine ni busara tu kutumika, kwamba wewe ni askari wa usalama barabarani, si lazima kusimamisha gari kukagua, isipokuwa kama umesikia pengine kwa njia za kiintelijensia kuwa gari fulani lina matatizo au barabara fulani ina matatizo hapo jitokeze.

Lakini kinyume cha hapo, bila shaka kwa uraibu huu, hata askari Magereza wataanza kupita majumbani kusaka wafungwa watarajiwa, huku na wa Zimamoto wakisaka majengo yanayotarajiwa kushika moto. Tuwapange tu vizuri matrafiki, wengi kwa kweli wanafanya kazi nzuri bado. Isipokuwa wachache wanaoweza kudhibitiwa.

**Alamsiki!**

# Familia mhimili katika kufanikisha sensa

Na Dk. Enock Mlyuka

AGOSTI 23, mwaka huu, Tanzania inatarajiwa kufanya sensa ya watu na makazi, mchakato ambao ni muhimu sana kwa maendeleo ya taifa.

Kutokana na kuwapo kwa jambo hilo, taasisi mbalimbali za kiserikali, binafsi na asasi za kiraia, zimekuwa zikihamasisha Watanzania kushiriki kwa nia ya kupata takwimu sahihi kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Sensa ya watu na makazi nchini, hufanyika kila baada ya miaka 10. Na tangu kuasisiwa kwa Muungano wa Tanzania, tayari zimefanyika sensa tano katika miaka ya 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), sensa ya watu na makazi ni utaratibu wa kukusanya, kuchambua, kutathmini, kuchapisha na kusambaza takwimu za kidemographia, kiuchumi na kijamii kuhusiana na watu wote na makazi yao katika nchi kwa kipindi maalum.

Kwa lugha nyingine, sensa ni mchakato maalum wenye lengo la kupata idadi ya watu wote katika nchi, umri,jinsia, mahali wanapoishi, hali ya elimu na ajira, hali ya vizazi na vifo na hali ya makazi. Kwa mantiki hii, sensa si jambo la kukaribisha laana na mkosi katika familia, bali ni suala la heri na baraka kwa familia, jamii na taifa.

Takwimu hizi za sensa ya watu na makazi zinaweza kuibua mahitaji halisi ya wananchi yakiwamo makundi maalum yenye uhitaji maalum kwa mfano, watu wenye ulemavu, wanawake, watoto, vijana na wazee. Kwa mantiki hiyo, sensa itarahisisha uandaaji wa sera na mipango ya maendeleo kulingana na uhitaji na mazingira yaliyopo.



### FAMILIA MHIMILI

Kutokana na umuhimu wa jambo hili na ili kufanikisha mchakato huo, familia ni nguzo kubwa kwa kuwa mkazo wa sensa ya watu na makazi unahusu familia moja kwa moja. Familia, kwa maana ya kaya, ndizo zenye takwimu sahihi na muhimu katika kufanikisha suala zima la sensa.

Kwa mantiki hiyo, familia zisiwafiche watu wenye ulemavu kutoshiriki katika kuhesabiwa kwa kuwa kufanya hivyo ni kinyume cha haki za binadamu na kosa la jinai. Mtu kuwa na ulemavu hakumwondolei haki zake za kiuchumi na kijamii ikiwa ni pamoja na haki ya kuhesabiwa.

**Sensa ya watu na makazi ni jukumu la familia kwa ajili ya familia, jamii na taifa kwa sababu familia ni serikali ya nyumbani ambayo ni msingi wa jamii na taifa. Bila familia hakuna jamii na taifa.**

Mtu mwenye ulemavu ni binadamu kama walivyo binadamu wengine wenye haki ya kuthaminiwa, kushirikishwa na kuhusishwa masuala yanayohusu maisha yao na taifa lao.

### JUKUMU LA FAMILIA

Kama ilivyobainishwa awali, sensa ya watu na makazi ni jukumu la familia kwa ajili ya familia, jamii na taifa kwa sababu familia ni serikali ya nyumbani ambayo ni msingi wa jamii na taifa. Bila familia hakuna jamii na taifa.

Kwa mantiki hiyo, familia zikiwa imara, kutakuwa na jamii na taifa imara. Familia ni chimbuko la uhai, shule ya upendo, maadili na uwajibikaji. Familia nyingi zinapitia changamoto mbalimbali za kisiasa, kiuchumi kijamii, kimazingira, kisheria, kiteknolojia, kimaendeleo na kiroho.

Ni katika muktadha huu, familia zote nchini zinahimizwa kushiriki sensa ya watu na makazi ili serikali iwafahamu watu wake na hali halisi ya mahitaji yao ikiwa ni pamoja na kufahamu umri, jinsi, uhusiano, na hali ya ndoa kwa maendeleo ya familia zenyewe, jamii na taifa. Familia zinapaswa kufanya makazi yao kuwa nyumbani. Nyumbani ni mahali ambapo ndugu na wanafamilia wanapaswa kushangilia ukarimu, wema, furaha, uwazi, uelewano, ukweli, upendo, kukosoana kindugu na kusaidiana.

Sensa ya watu na makazi msingi wake ni Mungu mwenyewe. Tangu enzi za manabii na mitume watu walihesabiwa ili watambulike na kufahamu idadi yao; kufahamu mahitaji yao halisi kwa ajili ya huduma mbalimbali na maendeleo. Mungu ni wa mipango na utaratibu.

Mungu alipoumba ulimwengu, aliweka utaratibu wa kutunzwa na kulindwa. Wanadamu wote wamepewa jukumu la kutunza, kulinda uumbaji wa Mungu na kuwa chimbuko la maisha yenye furaha. Hata hivyo, mwanadamu amepoteza wajibu aliokabidhiwa na Mwenyezi Mungu katika kutunza na kustawisha ulimwengu kwa faida yake mwenyewe. Kutokuwajibika ipasavyo na kukosekana kwa uwiano wa kijamii na kiuchumi kumekuwa ni chanzo cha mateso na mahangaiko.

Maendeleo ya nchi lengo lake ni kulinda uhai na kustawisha maisha ya watu wake. Uhai na ustawi wa afya zetu ni sehemu ya uumbaji wa Mungu na ajenda ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kwa hiyo, sensa ya watu na makazi itaiwezesha serikali kupanga mipango ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa ajili ya ustawi wa familia na wananchi wote.

Hali kadhalika, taarifa za idadi ya watu husaidia katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ambayo huakisi matakwa ya watu na uwiano wa mgawanyo wa rasilimali nchini.

Kuhesabiwa ni sehemu ya utambulisho. Kuzaliwa na kuishi tu haitoshi, bali kuishi na kutambulika ni muhimu sana. Watu ili washiriki mema ya nchi yao ni muhimu watambulike.

Sensa ya watu na makazi inatoa utambulisho wa pekee kwa familia. Kwa mantiki hii, familia zote zinaalikwa kuwapo nyumbani Agosti 23, 2022 ili kuhesabiwa na kutambulika kwa faida ya familia zenyewe na maendeleo ya taifa, ambapo wewe na mimi ni sehemu yake. Familia katika kaya zote zinao wajibu wa kuhesabiwa na kutengeneza mazingira rafiki ili kufanikisha zoezi hili.

### WAZAZI NA WALEZI

Wazazi na walezi ni walimu wa kwanza wa familia. Wazazi na walezi wanao wajibu wa kuelimisha, kuhimiza na kuandaa familia zao kwa ajili ya sensa ya watu na makazi. Wazazi wanaopenda familia zao hawatakwepa na kupuuzia wajibu huu. Familia ni kitovu na taasisi ya malezi endelevu.

Katika familia wazazi au walezi wanapaswa kuendelea na jukumu la kuwarithisha watoto wao tunu msingi wa matumaini, fadhila, uadilifu na uwajibikaji. Familia za wanadamu zinapotambua mpango wa Mungu maishani mwao, hujitengenezea mazingira salama na kuneemeshwa na Mungu.

Sensa ya watu na makazi ni muhimu kwa maendeleo ya taifa, hivyo ni muhimu wananchi na familia zote kushiriki ili taifa lijue idadi ya watu wake na kupanga mipango ya kuweza kuwahudumia vizuri zaidi.

Ili kufanikisha azma njema hii ya serikali, wale wote waliopewa dhamana ya kusimamia jambo hili wahakikishe kazi hii inafanyika kwa ufanisi ili kupata takwimu bora na halisia. Tanzania bora na imara itajengwa na Watanzania wenyewe kila mmoja atakapotimiza wajibu wake ipasavyo.

### JIANDAE KUHESABIWA

**Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

**Familia ni nguzo kubwa kwa kuwa mkazo wa sensa ya watu na makazi unahusu familia moja kwa moja. Familia, kwa maana ya kaya, ndizo zenye takwimu sahihi na muhimu katika kufanikisha suala zima la sensa.**



# MAISHA

JULAI 31, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 12



Ukurasa 13

**TOKA 'SIMPO' UTAPENDEZA**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Mambo ya kuzingatia unapotafuta ardhi kwa ujenzi





## PUA INAYONG'AA

## Mikono yako inaweza kukusaidia

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | L | A | A | N | A |
| | A | | | Y | |
| M | W | A | | U | |
| | A | | I | N | A |
| | M | | | G | |
| S | A | U | M | U | |

## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
IBA, ONA, YANGA, DIMBA, DONYOA, BAMBIA


## TOA TOFAUTI 5




## PAKA RANGI



## AMSHA AKILI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Suzana akiwa varandani na mama yake akimsaidia kazi za nyumbani. Wakati wakiendelea na kazi Suzana alimuuliza mama yake.

**Suzana:** Mama naomba nikuulize kitu kuhusu bahari

**Mama Suzana:** Sawa niulize tu

**Suzana:** Eti kuna samaki anayeitwa Nguva anafanana na binadamu, tena mrembo kama malaika?

**Mama Suzana:** Hakuna samaki wa aina hiyo

**Suzana:** Kumbe wanatuongopea hakuna samaki Nguva?

**Mama Suzana**: Samaki Nguva yupo lakini hana umbo la binadamu, hayo ni mapokeo na hadithi tu.

============

**SWALI**

Swali; Paa ni jamii ya Mnyama gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Umewahi kuchunguza matatizo yako king'ang'anizi?

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na vimbwanga vya safu hii. Hapa tunaelimishana kuhusu vituko au visa vya kimaisha ambavyo watu wengi wanakumbana navyo kila uchao kwenye familia zao.***

Maisha ni dhana pana iliyosheheni mambo mengi yakiwemo ya kiuchumi katika muenendo mzima wa binadamu hapa duniani. Ni misukosuko, purukshani, majanga, huzuni, furaha na kadhalika.

Leo nimulike wale ambao wana matatizo ving'ang'anizi lakini wanachukulia ni kawaida au kana kwamba ni sehemu ya maisha yao. Kumbe liko chimbuko au asili kwenye ukoo walikoanzia wazazi wetu.

Yamkini, wengi leo wanateseka kwa sababu tu hawarudi nyuma kudadisi historia ya chimbuko la familia zao. Kila familia ina waasisi na wakishakufa huwa wanajulikana kama wahenga.

Ziko familia ambazo zimejengwa katika msingi ya kiroho, yaani wacha Mungu. Pia ziko ambazo misingi yake ni kuabudu mizimu, matambiko, uganga na ushirikina. Isitoshe, ziko familia hadi leo zinaishi kwa kuzingatia maagizo, maelekezo au maagano yaliyowekwa na waasisi wake. Ni kama viapo ambavyo havipaswi kuvunjwa kwani viliambatana na masharti.

Kipo kisa kimoja katika moja ya maandiko ya Mungu kupitia Nabii Yeremia, akiagizwa na Mungu aende nyumbani kwa Warekebi akanene nao na kuwaleta nyumbani kwa BWANA katika chumba kimoja, akawape divai wainywe.

Nabii Yeremia akafanya kama alivyoagizwa na Mungu akawaleta ndani na kuweka mabakuli yaliyojaa divai na vikombe mbele ya wana wa nyumba ya Warekabi akawaambia wanywe divai. Lakini wakasema; Hatutakunywa divai; kwa maana Yonadabu, mwana wa Rekabu, baba yetu alituamuru, akisema, Msinywe divai, ninyi wala wana wenu, hata milele.

Wala msijenge nyumba, wala msipande mbegu, wala msiwe nayo; bali siku zenu zote mtakaa katika hema; mpate kuishi siku nyingi katika nchi ambayo mtakaa ndani yake hali ya wageni.

Nasi tumetii sauti ya Yonadabu, mwana wa Rekabu, baba yetu, katika yote aliyotuamuru, kwamba tusinywe divai siku zetu zote sisi, na wake zetu, na wana wetu, na binti zetu Wala tusijenge nyumba za kukaa, wala hatuna shamba wala konde, wala mbegu. Bali tumekaa katika hema, nasi tumetii, tukafanya sawasawa na yote aliyotuamuru Yonadabu, baba yetu".

Msomaji wangu, angalia familia hii, pamoja na kwamba Mungu aliweka mpango mzuri wa kuwaondoa katika hicho kifungo cha maelekezo ya baba yao ili wawe huru, lakini waling'ang'ania kutii walichoambiwa na Yonadabu. Wapo watu wanaishi kwa mateso leo kwa sababu tu ya kutoachana na maagano ya wahenga.

Wale waliotangulia katika familia zetu wengi hawakuweka misingi mizuri ya kiroho itakayowapa maisha mazuri vizazi vyao, badala yake wamewaachia mateso na kuwadumaza kimaisha.

Familia nyingi zimefungwa katika madhabahu za umasikini, ulevi, uzinzi, pasipo wao kujua. Hata wakijitambua hawajui wafanye nini ili waweze kutoka hapo walipo. Angalia familia ya Yonadabu imebaki hapo walipo kwa sababu ya kutii amri ya baba yao.

Kumbe wangeisikiliza sauti ya Mungu kupitia Nabii Yeremia wangejitambua na kuishi maisha ya neema na mafanikio aliyowakusudia Mungu mwenyewe.

Wapo watu wanataabika, ndoa zinaishia njiani, hakuna kuolewa, hakuna kuoa na hata wakibahatika kufunga ndoa zinavunjika. Wakioana hawapati watoto, watoto wanaishia darasa la saba, au sekondari. Hata akifanikiwa kufika na kumaliza chuo kikuu hawapati kazi.

Pamoja na matukio kibao yanayorudisha nyuma maendeleo ya watu wengi, bado hawachunguzi kujua chanzo. Yafaa kuchunguza waasisi/wahenga waliishije, walitamka maneno gani, walifanya maagano gani na kadhalika.

Pia katika maisha, yawezekana ilitokea mitafaruku kati ya wazazi, koo au uadui, au mauaji ambayo yaliacha matamko. Kwa mfano, utaona kama watoto wako wataoa au kuolewa, au baba alilaani wajukuu kwamba hawatakaa wafanikiwe, kisa eti wamekataa mkoba wa uganga na kadhalika. Maneno ni nguvu ni lazima yafutwe ili waliotamkiwa wawe salama.

Wapo ambao wamejikuta wao nguvu yao ya mafanikio inatokana na waganga wa jadi. Wazazi wake walikuwa washirikina na kila watakacho lazima waulizie kwa waganga. Wengi walijikuta wakiishia vibaya.

***Msomaji wangu, niishie hapa. Wiki ijayo nitakuletea kisa cha kimaisha cha kusisimua ambapo shangazi katika familia fulani alijifungua boga. Je, ilikuwaje na nini kiliendelea? Una maoni au kisa? Tuma ujumbe mfupi 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Jamii ichukue hatua kupambana na ulawiti, ubakaji

MATUKIO ya ulawiti na ubakaji wa watoto yanaongezeka kila uchao. Kesi nyingi zinadaiwa kuishia polisi au mtuhumiwa anapopewa dhamana familia zinakaa kuzungumza ili kuyamaliza kifamilia.

Aidha, baadhi ya vijana waendesha bodaboda wanadaiwa kuhusika na matukio hayo hasa wale wanaowabeba wanafunzi kuwapeleka shuleni kiasi kwamba wako watoto ambao wamefanyiwa ukatili na kuuzoea au kulazimishwa kuishi maisha ya mateso tangu wakiwa wadogo.

Kwenye shule za msingi na sekondari, matukio hayo yanaongezeka kwa watoto kufanyiwa hivyo na ndugu wa karibu ambao hulala nao wanapokaribishwa na mama, baba au mlezi baadae anashtuka mtoto ameshaharibika.

Aidha, inadaiwa fedha inatumika kumaliza kesi hizo na wakati mwingine madawati ya jinsia yamelalamikiwa kuwa sehemu ya uharibifu, ambao sasa ni maumivu kwa jamii.

Unapokwenda maeneo ya starehe, utakutana na vijana wa kiume wa rika mbalimbali wanajiuza yaani wanaingiliwa kinyume cha maumbile na wanaume wenzao, huku wasichana wakiwa na uhusiano na wasichana au wanawake wenzao.

Vitendo hivi vinaua kizazi kwa kuwa idadi ya wanaume inaendelea kupungua kila siku, huku takwimu zilizopo zikonyesha wanaume ni wachache ikilinganishwa na wanawake. Sasa linapotokea suala la ulawiti linapunguza idadi yao na kukiweka kizazi hatarini.

Inaelezwa kuwa mwanamume anapofanyiwa kitendo hicho, anatamani kuendelea kufanyiwa ndiyo maana wengi hujiuza ili kupata wa kuwafanyia hivyo. Hii ni kosa kisheria na limekatazwa na kulaaniwa kwenye vitabu vitakatifu vya dini.

Utafiti mdogo uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Mshataka ulibaini kuwa baadhi ya watuhumiwa wa makosa hayo wakiwa nje kwa dhamana, wanakimbia na wengine kuharibu ushahidi au kumalizana na wazazi ama ndugu wa mhanga wa vitendo hivyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Happy Msimbe, hivi karibuni alisema serikali imeanza mchakato wa kufanyia marekebisho Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, wanaanza mchakato wa makosa ya ubakaji na ulawiti kuondolewa dhamana. Katika kuonyesha ukubwa wa tatizo takwimu za Jeshi la Polisi, Tanzania katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2021, matukio ya ukatili kwa watoto yaliyoripotiwa ni 11,499, huku makosa yaliyoongoza kwa idadi kubwa ni ubakaji (5,899), mimba kwa wanafunzi (1,677) na ulawiti (1,114).

Aidha, mikoa iliyoongoza kwa matukio ya ukatili na idadi kwenye mabano ni Arusha (808), Tanga (691), Shinyanga (505), Mwanza (500) na mkoa wa kipolisi Ilala (489).

Baadhi ya familia zinamaliza kesi hiyo nyumbani, inapotokea mzazi mmoja anashikilia kuendelea na kesi mahakamani anaitwa na kukalishwa na ukoo, ikiwamo kutengwa kama atakubali kuendelea na kesi.

Wengi wanaokumbwa na kesi hizi wanatoka familia maskini ambazo wakati mwingine kufuatilia kesi ni usumbufu na gharama, wakati mwingine wanakutana na usumbufu mkubwa polisi na hospitali na kuamua kubaki nalo moyoni.

Wanaoteseka ni watoto na wazazi wao ambao wametendewa ukatili huo, lakini hawana pa kukimbilia kwa kuwa kila eneo hakuna msaada na mwisho matukio kuendelea kutokea.

Mabadiliko ya sheria hiyo kuongeza makali ni hatua nzuri sana kwa kuwa watu wataogopa na kesi zitashughulikuwa inavyotakiwa kwa kuwa ushahidi hautaharibiwa kama inavyofanyika sasa. Ni muhimu kulinda taifa dhidi ya ongezeko la mashoga ambao wanakuwa hivyo siyo kwa msukumo wa maumbile, bali kwa kufanyiwa ukatili na wachache ambao wananufaika au ni tamaa za mwili.

Lakini ni muhimu kuendelea kutoa elimu na kuchukua hatua mapema taarifa zinapotolewa, kuboresha madawati ya jinsia ili yasiwe kichaka cha rushwa na kuumiza watu, viongozi wa dini walio waadilifu kuendelea kuwahubiri yaliyomema waumini wao na kuwaonya kwa kutumia maandiko matakatifu juu ya vitendo hivyo.

Sheria kufanyiwa mabadiliko ni jambo jema, lakini bila kudhibiti rushwa ni sawa na bure kwa kuwa watu wataendelea kufinyanga kesi za namna hiyo, ili kupata fedha kwa waliotenda pasipo kuona uharibifu huo ipo siku utabisha hodi kwenye nyumba yake.

Kwa sasa tuna Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum, ambayo imeunda kamati mbalimbali kukabili vitendo vya ukatili, lakini ni muhimu kufuatilia hadi ngazi ya chini hasa kwenye shule za msingi na sekondari, lakini pia kuimarisha idara ya ustawi wa jamii, polisi na hospitali ili wafanye kazi kwa hofu ya Mungu na kuogopa kuyaharibu matukio hayo.

# 'SEND OFF'







ILIKUWA SIKU YA FURAHA KWA MARYPRISCA PATRICK, BAADA YA KUANDALIWA SHEREHE YA AINA YAKE YA KUMUAGA ILIYOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA NEW DELUXE, SINZA KIJIWENI, DAR ES SALAAM, JULAI 9, 2022.



MITINDO

Na Christina Mwakangale





# TOKA 'SIMPO' UTAPENDEZA

MAVAZI ni moja ya pambo linalomfanya mtu kuwa na muonekano tofauti.

Mara nyingi uchaguzi wa mavazi yanamfanya mtu kubadilika na kuwa mtanashati zaidi.

Hata hivyo, wanaume wanapenda kuwa watu wa haraka na mara nyingi hawatumii akili nyingi kuchagua mavazi.

Kutokana na sababu hizo, wanaume wanapenda kuvaa mavazi ya kawaida, hawajali sana mitindo, rangi au aina ya kitambaa.

Kama unapenda kuvaa kawaida, unatakiwa kuwa na nguo za rangi maalum ili kukupa urahisi.

Zifuatazo ni njia sahihi za kuvaa nguo za kawaida na ukapendeza.

**RANGI ZISIZO NA CHAGUO**

Kwa kawaida nguo za rangi nyeusi zinafaa kwa watu wasiotaka makuu. Nguo hizi iwe suruali au shati mwanaume anapovaa inamtoa bomba hasa akichanganya na rangi nyingine za nguo.

Mfano anapovaa Suruali nyeusi, shati ya rangi yoyote inamfaa na kumng'arisha zaidi.

Akivaa shati au fulana nyeusi, hatokuwa na kazi ya ziada kutafuta suruali kwani akivaa jeans, au suruali ya kitambaa ya rangi yoyote lazima itamtoa bomba.

**HALI YA HEWA**

Unachotakiwa kuwa mwangalifu namna ya kuvaa nguo na majira ya mwaka. Hapa unatakiwa kuwa makini licha ya kutoka 'simpo' ili kuepusha usumbufu.

Wakati wa kipindi cha joto, unatakiwa kuvaa nguo zinazoruhusu mwili kupumua, hivyo usivae nguo nzito zinazovaliwa kipindi cha baridi kwa ajili ya kukupa uhuru wa kutembea.



UREMBO

Na Mary Geofrey



# PUA INAYONG'AA

## Mikono yako inaweza kukusaidia



RANGI nyeupe inayoonekana kwenye ngozi ya juu ya pua ni dalili ya seli zilizokufa baada ya kukutana na hewa.

Vipele hivyo vidogo ni aina ya chunusi na huwatokea zaidi watu wenye ngozi za mafuta, wanawake kwa wanaume.

Unaweza kuviondoa kwa njia za asili ambazo kila mmoja anaweza kufanya hivyo akiwa nyumbani kwake.

Unachotakiwa ni kuosha uso wako mara mbili kwa siku na maji ya uvuguvugu.

Baada ya kuosha, fanya kama unapigapiga taulo usoni usisugue. Hii ni njia inayopunguza uchafu na mafuta kujijenga kwenye mashimo ya ngozi.

Mvuke ni njia nzuri ya kuondoa vipele, Unachotakiwa kufanya ni kuchemsha maji na kisha uyamimine kwenye bakuli.

Acha mvuke ukupige usoni kwa muda wa robo saa. Hii ni njia nzuri ya kufungua tundu au vinyweleo kwenye ngozi inakuwa rahisi kuondoa uchafu kwenye ngozi.

Ukitoka kuoga, tumia vidole vyako viwili kusugua taratibu eneo la pua, itaondoa ngozi zote zilizokauka.

Epuka kujishika eneo hilo wakati wote kwa sababu vijidudu vilivyopo kwenye mikono vinasababisha hali hiyo kuendelea au kuongezeka.

Unaweza kutumia njia nyingine ukiwa nyumbani kuondoa vipele hivyo.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Rosti ya 'Egg Chops' za nazi

ROSTI ni aina ya mboga iliyoungwa vizuri na kukolea viungo na kuwa katika hali ya uji mzito inaweza kuliwa na chakula cha aina yoyote.

Kuna rosti za aina mbalimbali za mboga mfano rosti la nyama, maini, samaki, kuku au aina nyingine ya kitoweo.

**Mahitaji**

Vijiko viwili vya mafuta ya kupikia, kitunguu maji kimoja, nyanya mbili, pilipili kichaa mbili,

Kijiko kimoja cha chai, kitunguu saumu na tangawizi.

Pia kijiti cha mdalasini, karafuu punje nne,Iliki punje sita, kijiko kimoja cha chakula kari poda, kijiko kimoja cha chakula unga wa nyama ya kusagwa na nusu kikombe tui la nazi.

Nusu kikombe cha cooking cream, chumvi kwa kuonja, majani ya giligilani, dania, kotimiri kiasi na egg chops nne.

**Namna ya kupika**

Weka nyanya, kitunguu maji na pilipili kwenye mashine ya kusagia chakula kutengeneza rojo.

Weka sufuria katika moto wa wastani, chemsha mafuta kisha weka kitunguu saumu na tangawizi, mdalasini, karafuu na iliki na kaanga mpaka harufu ya ubichi iishe na vilainike, kama dakika mbili.

Ongeza rojo ya nyanya iliyo na kitunguu, pilipili, na kari poda na kisha changanya vizuri, halafu funika.

Acha mchanganyiko uive katika moto wa chini kwa dakika sita hadi nane, au mpaka nyanya na viungo viive vizuri kabisa.

Ongeza tui la nazi na maziwa, weka chumvi na pika kwa moto wa chini kiasi kwa dakika kama tano.

Ongeza majani ya kotimiri, dania, giligilani halafu uweke eggy chops taratibu, geuza zipate kuchanganyika na uji pande zote na kuwa makini zisiharibike.

Acha mchanganyiko uive kwa dakika kama mbili nyingine na rosti yako itakuwa tayari kwa kuliwa.



## MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Mambo ya kuzingatia unapotafuta ardhi kwa ujenzi wa nyumba yako

KUTAFUTA ardhi ni hatua ya awali ambayo mtu hufanya katika kuelekea kujenga nyumba ya ndoto yake bila kujalisha mahali alipoipata.

Hata hivyo, kuna mambo ya msingi ya kuzingatia na kinyume chake unaweza kujikuta unapata ardhi na kujenga mahali ambapo mwisho wa siku itakuwa majuto kwako.

Mtaalamu wa ujenzi, Tamiko Hatula, anasema kuna mambo ya msingi unapochagua eneo la kujenga ambayo unapaswa kuyazingatia.

Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na kufanya uchunguzi wa historia ya eneo husika unalotaka kununua na kuangalia ufikikaji wake.

"Kiwanja chenye barabara pande zote huhusiana na furaha, afya njema na mafanikio, huwa na hewa, mwanga na nafasi ya kutosha. Kwa kiwanja kisichokuwa na barabara pande zote ni muhimu kuwe na barabara upande wa kaskazini au mashariki. Sababu ya msingi ni kwamba nyumba itakayojengwa itakuwa na mwanga na hewa ya kutosha kuanzia asubuhi," anasema.

Jambo lingine ambalo anashauri kuzingatia wakati wa kutafuta kiwanja kwa ajili ya ujenzi ni pamoja na kuhakikisha eneo unalonunua kwa ajili ya makazi au biashara na makazi.






"Hii itakusaidia uepukane na usumbufu wa kubomolewa au kuwa na hofu ya kuhamishwa, hakikisha unafuata taratibu zote za umiliki wa ardhi zilizowekwa," anasisitiza.

Hatula anashauri kuepuka kununua kiwanja kinachouzwa na mtu aliyepatwa na dhiki au kufilisika kwa kuwa baadae kinachangia kukukosesha furaha na amani.


"Kiwanja cha namna hii ni muhimu kinunuliwe kwa uangalifu mkubwa kwa sababu endapo utanunua kwa lengo la kujinufaisha zaidi, kitakufanya baadaye ukose furaha na amani. Manung'uniko yatokanayo na muuzaji au jamii inayozunguka yatachangia kukuondolea heshima na utu," anabainisha.

Anashauri kuepuka kiwanja kilicho jirani au kinachopakana na maeneo ya mikusanyiko mikubwa ya kijamii ikiwamo kumbi za starehe, kanisa, msikiti, kiwanda, chuo, jeshini, shule, soko, sehemu ya stendi za magari.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, maeneo hayo huwa na kelele nyingi na mara nyingi matumizi yake huathiri maeneo yaliyo jirani, ikiwamo kubadilishwa kwa matumizi wakati wowote na pia ni vigumu kulea watoto na kuwakuza kimaadili katika maeneo hayo.

Mengine, anayoshauri kuzingatia ni kuepuka kununua eneo linalomilikiwa au lililomilikiwa na taasisi za kiimani, eneo lililo jirani na sehemu ya taka, lenye magofu mengi, mapingamizi, nyufa na mipasuko pamoja na udongo wa mfinyanzi.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
NISHAJIPIGA 'SPIDI GAVANA' WE NJOO UTANIKUTA
SUBIRI KUHESABIWA
.......
.......
MZURU-RAJI
STAILI HII MGUUNI WAZARAMO WANAIITA 'MWANATUMBILI' WAULIZE WAPENDA KUSHOBOKEA KOMBE LA BWANA HARUSI
NYIE JISHAUENI LAKINI SIKU YA SENSA TUNAPAKI KUSHIRIKI ZOEZI MPAKA LIISHE
UKIMALIZA KUSHIRIKI UTATUKUTA NA SISI TUSHAMALIZA KA'WEWE
JAMANI NIMEKAA KIMYA SIO MJINGA ILA ATAKAYE-POTOSHA 'MAJI ATAITA MMA'
ANAONGEA KIASI KWAMBA HAJUI KITU WAJIBU
HICHO NDICHO UNACHOKIJUA! KUONEA WALEVI
JANAMKE LINA-GUBU UTADHANI NIMEOA REDIO YA MIPASHO! SASA HANIONI MWAKA WOTE
NIPO MASAA 24 HADI 48 BY BOSI
NIMEACHA POMBE NANYWA BIA TU
NIMEACHA ZINAA NACHEPUKA TU
MKE WANGU WATU WANAKU-ONA SANA STATAS UMEPAJUAJE?
NDIO KWETU
HE! HATA KAMA NAKARIBISHWA OFISI MPYA LAKINI SIO KUKARIBISHWA NA HUU MNARA!
KERO
...KINYUNYIZO CHA LEO...
UTAPOKEA VYETI LAKINI CHA KIFO CHAKO UTAPOKELEWA...

# Bil. 43/- kutekeleza vipaumbele jinsia

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dk. Dorothy Gwajima, amesema katika bajeti ya 2022/23, wizara yake inatazamiwa kwenda na vipaumbele vinane vitakavyotumia Sh. bilioni 43.3 iliyopitishwa na Bunge.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Dk. Gwajima alivitaja vipaumbele hivyo kuwa ni pamoja na kuratibu afua za kukuza usawa wa kijinsia, uwezeshaji wanawake kiuchumi na kiuongozi na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake, watoto na wazee.

Pia alisema kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoibuliwa ngazi ya jamii sambamba na kutambua na kuratibu makundi maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo (Machinga) ili kuboresha mazingira ya biashara zao. Waziri huyo alisema maeneo mengine ya vipaumbele ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii.

Kadhalika alisema kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwa watu wenye mahitaji maalum, huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia na huduma ya msaada wa kisaikolojia kwa manusura wa majanga mbalimbali na makundi mengine yenye uhitaji katika jamii.

"Wizara itaratibu na kuwezesha upatikanaji wa huduma za ustawi wa jamii kwa wazee, kuratibu na kusimamia afua za upatikanaji wa haki za mtoto, ulinzi na malezi chanya ya watoto sambamba na kuimarisha ushiriki na mchango wa mashirika yasiyo ya kiserikali katika maendeleo ya Taifa," alisema.

Kuhusu fedha za utekelezaji, Waziri Gwajima alisema Sh. bilioni 43.4 zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha uendeshaji wa ofisi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

"Wizara itatumia Sh.milioni 160.2 kuhamasisha jamii katika kujenga moyo wa kujitolea, uzalendo na kushiriki katika shughuli za maendeleo na Sh. milioni 107.1 kuandaa mwongozo pamoja na kuwajengea uwezo viongozi wa machinga kwa mwaka 2022/23," alisema Waziri.

Alisema Sh. bilioni 45 zimetengwa kwa ajili ya kundi la machinga ili kuendeleza ujenzi wa miundombinu kwenye masoko na kuwawezesha kupata mitaji ya kuendeleza biashara zao. Alibainisha maeneo mengine ya vipaumbele na fedha zitakazotumika ni pamoja na Sh. bilioni 5.3 kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwenye vyuo vilivyo chini ya wizara.

"Shilingi 24,950,000 zimepangwa kutumika ili kukamilisha Mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia pamoja na Mkakati wake, Shilingi 15,940,000 zitatumika kusambaza Mwongozo wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi.

"Shilingi 81,200,000 imepangwa kutumika kutekeleza ahadi za nchi kuhusu Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa katika eneo la haki za kiuchumi kwa wanawake," alisema.

Dkt. Gwajima ameendelea kufafanua kwamba, kwa mwaka wa fedha 2022/23 Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendesha kampeni kubwa ya jamii ya kupinga na kutokomeza ukatili inayoenda kwa jina la Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA), ambapo takriban watu 8,000 wameshajiunga nchi nzima hadi kufikia Julai 29, 2022.

Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Amon Mpanju, alisema jukumu kubwa la wizara ni kwenda kuweka msukumo wa utekelezaji wa bajeti hiyo iliyopitishwa na Bunge.

## Vijana wahitaji mkopo kuongeza uzalishaji mikate

**Na Steven William,** MUHEZA

ZAIDI ya Sh. milioni 30 zinahitajika kuboresha uzalishaji katika kiwanda cha kutengeneza mikate cha Wazo Jipya wilayani Muheza kwa ajili ya kununua mashine ya kutengeneza mikate na jenereta.

Hayo yalisemwa juzi na meneja wa kiwanda hicho, John Simon, wakati akimweleza Mbunge wa Muheza, Hamisi Mwinjuma, alipotembelea kukagua uzalishaji wa mikate katika kiwanda hicho.

Alisema awali walikopa Sh. milioni sita kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kwa ajili ya kufungua kiwanda na mpaka sasa wamerejesha Sh. Milioni tatu.

Kutokana na msaada huo, aliishukuru halmashauri kwa kuwa fedha hizo zimewawezesha vijana ambao wameanzisha kiwanda hicho na kwamba mpaka sasa kimefikia hatua nzuri ya uzalishaji.

Simon aliishukuru pia serikali kupitia Rais Samia Suluhu kwa kusaidia vijana kupata mkopo wa asilimia 10 kutoka halmashauri.

Mbunge wa Muheza, Mwinjuma, maarufu kama 'Mwana FA' alisema kikundi hicho cha vijana kimefanya jambo la maana kwa kuwa vijana wengi wakipata mkopo wanakimbilia kununua pikipiki za bodaboda.

Aliahidi kuwaunga mkono kwa kuwapigia debe wapate tena mkopo halmashauri ili kuongeza kununua mashine ya kisasa.

Mwinjuma pia alisema mpaka kufikia mwaka huu, halmashauri imetoa Sh. milioni 500 kutoka mapato ya ndani kwa ajili ya kukopesha vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu na mikopo hiyo inasaidia wajasiriamali.



Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, Sahil Nyanzabara, akifungua bomba la maji, kuzindua mradi wa maji wa Kitwana Ngogwa, uliotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), kwa ajili ya kuanza kutoa huduma kwa wananchi wa kata ya Ngogwa, Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Wauzaji vibao vya anuani na makazi kushughulikiwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

KIONGOZI wa mbio za Mwenge Kitaifa, Sahil Nyanzabara amesema yeyote atakayebainika kung'oa vibao vilivyowekwa na serikali vya anuani na makazi na kuviuza kama vyuma chakavu atachukuliwa hatua za kisheria.

Aliyasema hayo jana wakati akitoa ujumbe wa Mwenge wa Uhuru Kitaifa muda mfupi baada ya kuweka jiwe la msingi katika Ofisi ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.

Alisema mwananchi atakayebainika kuviondoa vibao hivyo barabara na kwenye makazi ya watu atawajibishwa kisheria ili iwe fundisho kwa wenye tabia kama hizo.

Nyanzabara alisema kuwa mataifa mengine yaliyoendelea kwa asilimia kubwa wanatumia anuani za makazi katika kuagiza vitu mbalimbali na mahitaji wanayoyahitaji wanayapata kwa wakati hivyo hivyo kuwapo kwake kuna umuhimu mkubwa na serikali imetumia gharama kuviweka.

Kiongozi huyo alitumia nafasi hiyo kuhamaisha wananchi kujitokeza kwa wingi kuhesabiwa wakati wa Sensa ya Watu na Makazi inayotarajia kufanyika Agosti 23, mwaka huu ikiwa ni pamoja na kutowaficha watoto wenye ulemavu.

Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba, alisema Wilaya hiyo imekuwa ikiendelea na ujenzi wa miundombinu hivyo bila kuwapo kwa anuani za makazi itakuwa ngumu kuwaelekeza maofisa wa zima moto pindi majanga ya moto yanapotokea.

MAKALA

# MKOSEE ILI UMJUE



Na Magabilo Masambu - 0689157789

LAKINI mimi nawaambia, kila mtu amwachaye mkewe isipokuwa kwa habari ya uasherati, amfanya kuwa mzinzi na mtu akimuoa yule aliyeachwa azini." Hayo ni maneno kutoka maandiko matakatifu juu ya masuala ya ndoa. Lakini siku za hivi karibuni pamekuwapo na taarifa nyingi kila kona ya nchi zihusuzo mauaji ya wanandoa au wenza na bado taarifa hizo zinaendelea kuripotiwa.

Sababu zinazotajwa ni nyingi lakini kwa kiasi kikubwa inaelezwa ni kutokana na wivu wa mapenzi. Wengine wanadai hata ugumu wa maisha unaweza kuchangia lakini matukio haya yamekuwa pia yakiwahusisha watu wenye fedha nyingi. Pengine nayo ni sababu kwamba mtu anasema ana pesa na anaweza kumfanya mtu mwingine chochote.

Binafsi naweza kutofautiana na wengi, nadhani huwa yanafanyika makosa nyakati za mwanzo kabisa watu wanapoanzisha uhusiano. Siwezi kusema kuwa ni sababu tosha ya haya yanayotokea lakini kwa asilimia kubwa, inaweza kuwa hivyo.

Mapenzi mapya huwa yanatawaliwa na unafiki wa hali ya juu kuliko uhalisia. Kila mmoja anajitahidi kuonyesha upendo wa hali ya juu. Taarifa nyingi za mtu huwa zinafichwa kwa ustadi mkubwa huku mambo yakionekana yanakwenda barabara.

Lakini nataka niseme kama unataka umjue mtu uliye naye ni wa aina gani, ana uvumilivu wa kiwango gani, ana hasira kiasi gani, basi huna budi umkosee katika siku za mwanzo kabisa za uhusiano wenu. Kwa maana nyingine unaweza kutomkosea lakini ukaamua kuuishi uhalisia wako.

Inawezekana bado pamoja na kuishi uhalisia au ukamkosea asionyeshe ni mtu wa namna gani kwa mwenye akili hata ile kukubaliana na makosa yako utaweza kujua. Bahati mbaya hatutaki kufanya hivyo siku za mwanzoni kwa hofu ya kupoteza uhusiano ambao pengine tumeusubiri kwa miaka mingi lakini baada ya muda uhusiano huo ukachangia wakati mwingine mpaka mauti yetu.

Kumjua mtu ninakozungumzia hapa si kuzijua tabia zake bali kumjua anavyoweza kukabiliana na matokeo ya tabia.

Tabia za mtu ni jambo moja na namna ya kukabiliana nazo ni jambo la pili. Hili la pili ndilo linalowashinda wengi. Wako wanaozijua tabia za wenzi wao lakini wanajua pia namna ya kuzikabili katika njia ambazo hazileti mauti japo zinaweza kuleta athari za hapa na pale.

Mwanzoni nilianza na maandiko matakatifu kutoka kitabu cha Mathayo, yanayoeleza sababu kubwa ya kumwacha mwanamke japo hayaelezi juu ya mwanamume. Ujumbe wa jumla unaonyesha sababu pekee ya kupeana talaka ni uasherati.

Ni ukweli kwamba katika kuishi kwa wanandoa au wapenzi, yanaweza kuwepo mambo makubwa na mazito zaidi ya uasherati. Mfano, umegundua kwamba mwenza wako amefanya majaribio kadhaa ya kutaka kukuua na unao ushahidi usiotia shaka. Mtu huyu hajafanya uasherati, je, utasubiri mpaka afanye uasherati upate sababu ya kumtaliki? Najaribu kuuliza tu, sijasema ikitokea hivyo fukuza pengine bado unaweza kumsamehe na akabadilika na kuwa mtu mwema!

Sababu kubwa inatajwa ni wivu. Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kusema upumbavu ni kipaji kama ulivyo urefu na ufupi na kwamba ukishaumbwa hivyo ndivyo utakavyokuwa. Hata suala la wivu liko hivyo. Wivu hauigwi kutoka kwa mtu, kwa maana kwamba tabia ya kurithi kibaolojia na kisaikolojia tunaita "nature" yaani "genetic trait" na si tabia ya kimazingira (nurture). Kwa maana nyingine mtu mwenye wivu hawezi kubadilika kirahisi, hivyo mara zote anaona anaibiwa.

Yako maneno yanasemwa watu wenye wivu sana nao hawajambo kwenye kuchepuka! Hilo sina uhakika lakini kama ni kweli, kwa nini mara zote kabla ya kuwahukumu wenza wetu nafsi zetu zisituhukumu? Kwa maana imeandikwa kabla hujatoa kibanzi katika jicho la mwenzako, toa boriti kwanza katika jicho lako. Kabla hatujachukua hatua yoyote tujiulize je, sisi ni wasafi kiasi hicho? Au ndiyoo ile kwamba mwizi hapendi kuibiwa?

Wako wanaochanganya kati ya wivu na upendo wa dhati. Wanadhani kumfuatilia mwenza wako kila mahali ndiyo upendo huo. Si kweli. Wengine wanasema kama huna wivu, humpendi mwenza wako na hiyo si kweli.

Yote haya hayamaanishi msisimamie mambo ya msingi ndani ikiwa ni pamoja na kuleta heshima ya ndoa. Isije kuonekana kwamba ukirudi nyumbani usiku wa manane mwenzako asikuulize ulikuwa wapi eti kwa kufanya hivyo utakuwa wivu, isieleweke hivyo. Misingi ya ndoa inabaki pale pale na uhuru pia uwe na mipaka yake.

Ushauri wangu, maisha ni zaidi ya mapenzi. Fikiria mali ulizo nazo, watoto wako, ndugu na jamaa wanaokutegemea na taifa kwa ujumla halafu eti unafikiria upumbavu wa kuua mke au mume uliyekutana naye ukubwani. Bahati mbaya sana hukuwa hata wa kwanza kwakwe basi.

Kama mmeshindwana mnaachana tu kiroho safi. Eti unajiua, halafu mwenzako kesho anaolewa maisha yanaendelea. Huo ni ujinga. "Ohoo unajua nimegharimikia sana" ni mfugo huyo? Una tatizo basi. Pamoja na kugharimia kote huko, bado unaibiwa? Mpango wa Mungu ni watu tuishi si kuuana.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# 'Mahmoud' wimbo wa Msondo kisa 'demu' aliyempiga chini jana kiaina



Na Adam Fungamwango

LEO kwenye safu hii, tutaulezea wimbo wa JUWATA Jazz Band, maarufu kwa mtindo wa Msondo Ngoma, unaitwa 'Mahmoud'. Wimbo huu unaeleza tukio la kweli lililotokea miaka ya 1980 jijini Dar es Salaam. Ulitungwa na Joseph Lusungu, sasa marehemu.

Sauti safi zilikuwa zake yeye mwenyewe, Juma Akida, TX Moshi William na Nico Zengekala (wote hawa pia ni marehemu). Kisa hiki kilimtokea rafiki yake Lusungu ambaye alikuwa shabiki wa Msondo Ngoma.

Baada ya kukumbana na tukio hilo alimhadithia Lusungu na kama kawaida ya wanamuziki wa zamani, ukimhadithia kitu tu, au kikimtokea, ujue tayari anakwenda kukitungia wimbo.

Lusungu akatengeneza mashairi na kuyapeleka mazoezini. Ukafanyiwa mazoezi na marekebisho kidogo ndipo ukatokea wimbo huu wenye kisa cha kusikitisha, lakini pia ukaacha maswali mengi ya kujiuliza.

Ni kawaida ya mwanamume kumtokea au kumweleza mwanamke kuwa anampenda. Mwanamke naye akishapata ujumbe huo sasa ni hiari yake kujibu au kutojibu. \

Na kama kujibu atatoa jibu la aina gani? Anaweza kukubali au kukataa. Pia jibu moja kati ya hayo mawili linaweza kutoka siku hiyo hiyo, au likachelewa, na haijalishi litachukua muda gani. Haya ndiyo maisha ya wanadamu, mwanaume na mwanamke tangu enzi na enzi. Na hata mwanamke akikataa, mwanaume huwa hawezi kufanya chochote kile. Kwa sababu mapenzi siku zote ni ridhaa na si utumwa. Hebu twende kwenye wimbo wenyewe.

"Usiku wa Jumamosi ile, nikiwa Msondo Ngoma, kulia kwangu nilimuona, bibi Shakira, mwenye furaha, akiusakata Msondo. Nilishindwa kujizuia, nikajikuta bega kwa bega, nilimuomba nicheze naye, bila kusita alikubali, nikamueleza kuwa nimetokea kukupenda. Naye akanijibu, hapa nimefuata Msondo nijifurahishe, wasiliana nami kesho Keko Machungwa."

Tunaona kuwa jamaa alikwenda kuburudika kwenye bendi ya Msondo lakini wakati anacheza kulia kwake alimuona mrembo aliyeushtua moyo wake aliyekuwa akilisakata dansi.

Mahmoud akashindwa kujizuia katika kumuangalia, huku mwenyewe anacheza, akajikuta yupo mbele yake.

Kitendo bila kuchelewa anamuomba acheze naye, bibie akakubali. Hapo hapo jamaa akaingiza kete, akamwambia jinsi alivyomzimikia. Bibie akamjibu kuwa pale sipo mahala pake, kwa sababu alichofuata ni muziki, kucheza Msondo na jambo ambalo analihitaji au aliloiomba kama anataka majibu yake, awasiliane naye kesho maeneo ya Keko Machungwa.

Duru zinasema awali, Msondo waliimba, wasiliana nami kesho Polisi Ufundi. Lakini kama kawaida zamani mashairi kabla ya kurekodiwa yanapelekwa Redio Tanzania Dar es Salaam kufanyiwa masahihisho, kwa sasa watoto wa mjini wanaita 'editing'.

Maeneo yanayozungumzwa hapa ni Polisi Barracks, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam, sasa watu wa RTD kwa sababu ulikuwa wimbo wa mapenzi na jamaa na mwanamke wameahidiana kukutana maeneo ya Polisi Ufundi. Hawakuona kama kuna mantiki hata kama ni kweli kwa sababu hayo ni maeneo ya Jeshi la Polisi, hivyo isingekuwa vizuri kutumia jina la eneo hilo kukutania, wakaamua kuliondoa na kuwaambia watafute jina lingine.

Kwa ushiriakiano wa wanakamati wa RTD na wanamuziki wa Msondo, wakaamua kuweka neno 'Keko Machungwa' kwa sababu eneo hilo pamoja na kwamba linaitwa Polisi Ufundi, liko Keko Machungwa. Wimbo bado unaendelea na sasa anaimbwa Zengekala peke yake.

"Nilipofika Keko Machungwa, kama tulivyoahidiana na Shakira, nilimkuta, nikamweleza nia yangu tuwe wapendanao. Naye akanijibu kwa huzuni kubwa, huku akitabasamu. Nilikuahidi, samahani sana, kusema kweli kama nimeshindwa. Najua unanipenda ila nasikitika sana mama, nina mchumba wangu tutafunga ndoa karibuni. Ewe Mahmoud pole sana 'faza', pole kwa usumbufu ulioupata, ewe Josele Josele, pole sana 'faza' aa, pole kwa usumbufu ulioupata."

Wimbo huu ulikuwa na mashairi mengi sana, lakini hayo machache yalijitosheleza kabisa.

Jamaa alifika alipoahidiwa, na 'demu' naye akafika. Akaonyesha kujali kwa sababu alimwahidi afike hapo, wala hakumuacha kwenye mataa, akafika. Kilichotokea sasa.

Wakati jamaa anadhani kwa sababu mwanamke amefika, mambo yatakuwa mazuri, bibie anamwomba samahani nyingi. Anamwambia alimwahidi afike, lakini ukweli ni kwamba ana mpenzi wake watafunga ndoa karibuni. Anamwambia ni kweli anatambua kuwa anampenda sana lakini ukweli ndio huo. Anamuomba samahani kwa usumbufu alioupata.

Kwenye wimbo huu inaonyesha kuwa dada huyo ni mmoja wa wanawake wastaarabu sana kwa sababu hakumwongopea kitu chochote. Alimwahidi afike sehemu ile.

Angekuwa mwingine inawezekana kabisa asingekwenda na wala hakuna ambacho kingetokea. Demu akaenda na akamweleza ukweli wote, na samahani nyingi. Ni ustaarabu wa hali ya juu sana.

Lakini cha kujiuliza hapa ni kwa nini mwanadada huyo asingemweleza tu hayo siku ile ile pale Msondo wakati wanacheza muziki? Si wakati wanacheza na kuambiwa anapendwa angemwambia ni kweli lakini umechelewa baba kwa sababu nina mchumba wangu tunayetarajia kufunga ndoa karibuni?

Kwa nini amempatisha taabu na matumaini kibao kijana wa watu kumwambia tukutane sehemu fulani kesho huku akijua kitu anachokwenda kumwambia hakitokuwa rafiki kwake?

Kwa nini amtoe mbali kijana wa watu kwa lengo la kumtia tu presha? Au mwanamke huyo hakutaka kumwondoa kwenye 'mudi' Mahmoud siku hiyo walipokuwa Msondo, akaona kwa sababu ni sehemu ya furaha na kila mmoja anafurahia muziki?

Hakutaka kumnyong'onyesha ndiyo maana akamwambia wakutane kesho wakati kila mmoja yuko kwenye hali yake ya kawaida?

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na walipomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-12

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

MWANANGU jitulize, wewe ni msichana mzuri sana ujue, basi tu maisha yetu duni, umeshamaliza chuo, najua siku hizi ajira ni ngumu, lakini usijitumbukize kwenye masuala ya ajabu. Hawa vijana hawatokufikisha popote. Tulia, unaweza kupata kazi baadaye. Hakuna anayeweza kukupa kazi wakati ushakuwa mjamzito, ujauzito unatakiwa ukukute tayari una kazi yako na unajitegemea. Ukijituliza unaweza kupata mume wa kukuoa. Hakuna mwanaume atayemuona msichana kirukanjia akamfanya awe mkewe" Hasnat alikumbuka maneno ya mama yake aliyokuwa akimwambia mara kwa mara, alipomaliza tu chuo.


Na kweli alijituliza, akatulizana mtoto wa watu licha ya kwamba wavulana na kinababa walikuwa wakimuwinda kama simba anavyowinda swala porini, kwa ahadi nono, na hata vitisho pia, lakini wakaambulia patupu.

Leo hii anaona sura ya mtu katili aliyeingia akiwa na nia ya kuua, akighairi ghafla. Na hiyo ni baada ya kuona sura yake. Akaamini maneno ya mama yake kuwa ana uzuri wa asili. Na hata huo alionao ni nusu tu kwa sababu ya uduni wa maisha.

Akashuhudia mbwa mwitu amegeuka na kuwa njiwa. Hakujua cha kufanya. Alichosubiri kusikia ni nini mvamizi huyo ataongea.

Hidaya naye pamoja na woga wa kuuawa alijiuliza maswali mengi. Ni kwa nini kijana huyu aliingia ghafla na kutaka kuwaua? Tena kwa bastola? Anachojua ni kwamba Mwananyamala hakuna majambazi, bali vibaka. Vibaka huwa hawana bastola. Wachofanya ni kuingia kwenye majumba ya watu na mapanga, visu na bisibisi kama wanavamia nyumba za watu. Awe mmoja au wengi. Kama njiani basi watakupora, au kukukaba kabla ya kupora. Huyu kaingia na bastola ndani. Kwa nini atumie bastola ili kutaka kuiba vitu vyenye thamani ndogo tu na vya kawaida sana humo ndani.

Kwa jinsi anavyomuona si aina ya wale vijana wakabaji, wezi au vibaka, kwani alikuwa amevaa shati na suruali ya gharama ambayo si yoyote kati ya vijana wa kule ambaye angeweza kumudu kununua.




**Hidaya naye pamoja na woga wa kuuawa alijiuliza maswali mengi. Ni kwa nini kijana huyu aliingia ghafla na kutaka kuwaua? Tena kwa bastola? Anachojua ni kwamba Mwananyamala hakuna majambazi, bali vibaka. Vibaka huwa hawana bastola.**

Wajihi na sura vilikuwa tofauti na wale vijana au wezi anaowajua. Hakuonekana kuwa na shida ya senti mbili tatu. Alionekana kama anatoka kwenye familia bora.

"Nyumba kama hii yangu jamani, tena na bastola anakuja kuiba nini lakini?" Akajiuliza, lakini hakupata jibu.

Kichwa kilimuuma zaidi baada ya kuona kijana yule ameghairi utaratibu wote alioupanga. Hakujua ni kwa nini?

Amri zote alitii, alichobaki ni kumsikiliza tu mvamizi ni nini ataongea.

"Mama, samahani, naomba unisamehe sana. Mimi siyo mkosaji. Na wala siyo mtu mbaya kama ambavyo mlivyoona. Ila nikwambie ukweli kabisa kuwa niliingia kwenye nyumba hii siyo kuchukua kitu chochote kutoka humu." Akaanza kujitetea.

Hata hivyo si Hidaya wala Hasnat aliyeongea kitu chochote kwani kwa jinsi walivyotishika mara ya kwanza, bado nguvu zilikuwa zimewaishia. Na yote hayo yanayotokea bado hawakuamini na kuona kama ndoto hivi.

"Mimi siyo mwizi, na wala sikuja kuiba chochote humu ndani. Nilikuja kuua." Akasema na kuwafanya walio ndani ya hofu kuendelea kuwapo upya, japo aliongea kwa namna ambayo hakutaka kuwatisha tena.

"Lakini haikuwa amri yangu. Nimetumwa kuja kuua. Na nimetumwa kumuua mtu mmoja tu. Ni Hidaya ambaye ni wewe mama." Hidaya na binti yake jasho lilizidi kuwatoka wasielewe hata moja linaloendelea.

Ni kama vile aliona wasiwasi ukiendelea usoni mwao. Prince alinyanyuka na kuielekea meza. Akaiweka bastola yake katikati ya meza. Akarejea na kukaa pale pale alipokaa mwanzo pamoja na Hidaya.

"Nimeweka bastola pale ili msiwe na wasiwasi, msitishike. Nimesema sitowadhuru tena."

Baada ya Prince kuweka bastola, Hidaya alionekana kujikakamua na kuuliza swali, ingawa kwa woga.

"Kijana ni nani aliyekutuma kuniua na kwa nini umeahirisha?"

"Swali zuri mama. Kuna kitu ambacho ulikifanya zamani sana na wenzako, kwa hiyo nimetumwa kulipiza kisasi kwa wote. Wote nimewamaliza, ulibaki wewe. Na huenda ningemuua na binti yako kwa ajili ya kuficha ushahidi, lakini macho yangu yamenisaliti. Nimetokea kumpenda sana binti yako, muda mfupi tu niliomuona, kusema kweli nimevutiwa naye, kwa hiyo nimeahirisha kila kitu. Ninachoomba mama yangu kwanza unisamehe, nachotaka ni kumuoa binti yako."

Prince alitumia neno kuoa ili asikataliwe, kwa sababu isingewezekana kumuoa ghafla kiasi hicho. Alichotaka kwanza aruhusiwe awe mpenzi wake, lakini asingeweza kusema hivyo mbele ya mama yake. Pia tayari ameshaonekana ni kijana katili, muuaji.

Mapenzi ni kitu ambacho Hidaya anakifahamu vizuri mno. Huwa hayana wakati au sehemu, yanaweza kumea wakati au sehemu yoyote ile hata ndani ya maji. Alipoambiwa hivyo na hali aliyoiona tangu tukio lilivyoanza aliamini, aliona ni kweli kijana alikumbwa na hali hiyo, kwa vyovyote vile asingeweza kuongopa.

Kuiweka bastola mbali na kuomba msamaha, hata alivyokuwa akimwangalia sana binti yake, ilianza kumpa nguvu na kuanza kurejea kwenye hali yake ya kawaida taratibu japo si kwa asilimia zote.

"Baba, mimi siwezi kujibu au kusema kitu chochote kwa sasa. Hapa nilipo sina nguvu, miguu yote imekufa ganzi, hata kusimama siwezi, hapa nilipo naongea huku nahema, kwa hiyo siwezi kusema chochote kuhusu hilo kwa leo. Mpaka labda kesho na niwe na uhakika na hilo unalosema." Wakati huo, Prince alianza kumuangalia Hasnat kwa aibu na kumvizia, tofauti na alivyokuwa akimuangalia mwanzo. Hasnat yeye aliacha kumuangalia mvamizi, badala yake akawa anamuangalia usoni mama yake.

Aliingiza mkono mfukoni na kutoa kibunda cha noti za shilingi elfu kumi kumi. "Jina lako Hasnat vilee eee."

"Ndiyo" Akajibu kwa sauti ndogo.

"Chukua hizi. Ni shilingi laki mbili. Ni zako. Utakwenda kununua nguo. Ila siyo kesho, kesho nataka uwepo hapa nyumbani." Wakati huo tayari binti alikuwa amenyanyuka na kuzichukua, akarudi tena kutaka kukaa chini alipokuwa amekaa mwanzo.

"Hapana, kaa hapa." Safari hii akamtaka kukaa kwenye kochi upande wake wa kulia, huku kushoto akiwa Hidaya.

**ITAENDELEA JUMAPILI**

## HABARI BURUDANI



# PHYNO, TEKNO KATIKA UJIO TOFAUTI

MWANAMUZIKI na CEO wa Penthauze Music, Phyno ameibuka upya na ngoma kali inayoitwa 'Full Current' ambayo ndani kuna nyota mwingine wa Nigeria, Tekno.

Ngoma hiyo ambayo Phyno ametumia umahiri mkubwa kutaja sifa za kipekee za mpenzi wake, imepigwa katika miondoko ya Amapiano yenye mizizi yake Afrika Kusini.

Kwa Mwaka 2021 rapa huyo kutoka Nigeria aliachia albamu yake ya nne iitwayo SOMETHING TO LIVE FOR ambayo bado inafanya vizuri huku akitarajia kuachia nyimbo zingine mpya.

# Bella akerwa na wanaolazimisha ndoa



MFALME wa sauti katika muziki wa dansi, Christian Bella, amesema tabia za baadhi ya wanawake kutangaza ndoa baada ya kuishi na mwanaume miaka miwili haipendezi.

Amesema suala la ndoa lazima kujipanga kati ya mwanaume na mwanamke, lakini mashinikizo ya ndoa yanasababisha wapenzi wengi kutoelewana.

"Utakuta mwanamke umeishi naye miaka miwili anaaza kulazimisha ndoa, jambo hili halina maana kwani kila kitu kinakwenda na mipango lazima mjihakikishie mnakula na kuwatunza watoto mkiwazaa," amesema Bella.

Aidha, alionya baadhi ya mashemeji huenda wakawa chanzo cha kukwamisha ndoa nyingi za vijana kutokea kwa sababu wanakuwa na mahitaji mengi.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LAPORTA AFUNGUKA HATIMA YA DE JONG

**Bosi huyo atahadharisha katika soka huwezi kujua litakalotokea siku za mbele lakini...**

**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta amekiri atafanya kila awezalo kumbakisha Frenkie de Jong, lakini amekataa kuondoa uwezekano wa nyota huyo kwenda Manchester United.

Manchester United na Barcelona wamekubali ada ya euro milioni 85 kwa kiungo huyo, lakini mpango huo umesitishwa na msisitizo wa De Jong wa kulipwa karibu euro milioni 20 ya mishahara anayodai.

Laporta amezungumza kuhusu mustakabali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 katika wiki za hivi karibuni na mara nyingi amekuwa akisisitiza anataka Mholanzi huyo abaki Camp Nou, lakini alipoulizwa na CBS Sports kama anaweza kuthibitisha kwa dhati De Jong hataondoka, alikiri bado inawezekana.

"Kwenye soka huwezi kujua, siwezi kusema kimsingi, yote inategemea vyama tofauti. Lakini kimsingi, naweza kusema kuna uwezekano mkubwa akabaki, na naweza kusema kama rais nitafanya kila niwezalo kwa ajili yake, atabaki Barcelona," alisema Laporta.

Aliongeza: "Kitu cha kwanza kusema tunataka Frenkie abaki Barcelona. Tunampenda mchezaji huyo na yeye kama binadamu. Nataka abaki Barcelona. Ni mchezaji wa hali ya juu na mtu mzuri."

Alipoulizwa kuhusu hitaji la De Jong kukatwa mshahara, Laporta alisema: "Yote tunayofanya na Frenkie ni sawa na wachezaji wengine wa kikosi. Frenkie ana mkataba na tunaheshimu hilo hatuwezi kumlazimisha apunguze mshahara ni uamuzi wake.

"Tunajaribu kuisimamia klabu ya soka kwa busara na uendelevu, hivyo inabidi tufanye mazungumzo haya na tunayafanya kwa utulivu na kutafakari, tumeeleza hali ilivyo na tunashukuru kwa mchezaji yeyote ambaye anaweza kutusaidia.

"Ilikuwa hivyo kwa Dembele na ninamshukuru sana. Na baada ya mazungumzo ya miezi kadhaa, alikubali kujadiliwa upya kwa mshahara wake na anaweza kujivunia uamuzi wake.

"(Ikiwa De Jong hatapunguza mshahara) basi ataendelea. Ana mkataba. Tutaheshimu uamuzi huo. Kwetu sisi, yeye ni mchezaji wa Barcelona. Tunamtegemea."

## KWA UFUPI

### BOJA ATAJWA MADRID

KLABU ya Real Madrid wameuliza kuhusu kupatikana kwa mshambuliaji wa Chelsea na Albania, Armando Broja mwenye umri wa miaka 20, ambaye alicheza kwa mkopo Southampton msimu uliopita. (***Standard***)

### PAVARD ANUKIA CHELSEA

MLINZI wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Benjamin Pavard mwenye umri wa miaka 26 atakuwa tayari kujiunga na Chelsea ikiwa watatoa ofa nzuri. (***Bild***)

### WERNER KUREJEA LEIPZIG

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 26 amekubali kupunguzwa kwa mshahara kwa asilimia 50 ili kujiunga tena na RB Leipzig na ada ya mkopo yenye kipengele cha kununuliwa. (***Bild***)

### DEPAY ATAKIWA JUVENTUS

MCHEZAJI wa kimataifa wa Uholanzi na Barcelona, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 28 ni miongoni mwa wachezaji wanaolengwa na vigogo wa Italia, Juventus. (***Fabrizio Romano***)

### MARTIAL ANUKIA JUVENTUS

KLABU ya Juventus pia imeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufarasa, Anthony Martial kutoka Manchester United kwa mkopo, lakini kocha wa Mashetani Wekundu hao, Erik ten Hag anahitaji kumbakisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. (Calciomercato)

### SESKO KUTUA UNITED

KLABU ya Manchester United imekutana na wakala wa mchezaji wa Red Bull Salzburg, Benjamin Sesko kuhusu uwezekano wa kumnunua mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Slovenia mwenye umri wa miaka 19. (***Manchester Evening News***)

### CITY: HATUMUUZI SILVA

KLABU ya Manchester City imekanusha tetesi iko tayari kumuuza kiungo wa kati wa Ureno, Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 27 kwa Barcelona baada ya ripoti kueleza kuondoka kwake kunaweza kufadhili mkataba wa kumnunua kiungo wa kati wa Lyon na Brazil, Lucas Paqueta (24). (***Mail***).

### CASADEI AKARIBIA EPL

CHELSEA imetoa ofa ya kwanza kwa Inter Milan kwa ajili ya kumnunua kiungo wao wa kati wa Timu ya Taifa ya Italia, Cesare Casadei mwenye umri wa miaka 19. (Gianluca di Marzio)

### BARKLEY ATAKIWA EVERTON

EVERTON wamepiga hatua katika mazungumzo ya kutaka kumsajili tena kiungo wa kati wa England, Ross Barkley mwenye umri wa miaka 28 kutoka Chelsea, na pia wanataka kumchukua mshambuliaji wa Ubelgiji, Michy Batshuayi na kiungo wa kati wa Scotland, Billy Gilmour (21) kutoka klabu hiyo ya Stamford Bridge. (***90Min***)

### RODON ANUKIA SPURS

KLABU ya Rennes imekubali mkataba na Tottenham Hotspur kwa ajili ya kumsajili, beki wa Timu ya Taifa ya Wales, Joe Rodon mwenye umri wa miaka 24 kwa mkopo wa msimu mzima. (***90Min***)

### RAMSEY ATAMANI MAREKANI

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Wales, Aaron Ramsey mwenye umri wa miaka 31 anavutiwa na klabu za Ligi Kuu Marekani, MLS, baada ya kusitishwa kwa mkataba wake na Juventus. (***Mail***)

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI

PARIS ST GERMAIN
VERSUS
NANTES


1 | 1.36
X | 4.87
2 | 6.31

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# WERNER AKARIBIA KUTUA RB LEIPZIG



**LONDON,** England

RB Leipzig imefanya mazungumzo na mshambuliaji wa Chelsea, Timo Werner baada ya Mjerumani huyo kupewa ruhusa ya kujitafutia klabu mpya, kwa mujibu wa 90min.

Werner amekuwa hana wakati mzuri tangu ahamie Chelsea, akifanikiwa kufunga mabao 23 katika mechi 89 hadi sasa, na tayari ametangaza hadharani kusikitishwa kwake na kukosa muda zaidi ya kucheza.

Huku Kombe la Dunia likija baadaye mwakani, Werner anataka muda wa kucheza mara kwa mara na haamini ataupata pale Chelsea, na vyanzo vimethibitisha sasa anatafuta klabu mpya.

Chelsea wako tayari kuachana na Werner, tayari wamemnunua Raheem Sterling kwa dau la pauni milioni 47.5, na wawakilishi wake wamempa ofa kwa timu kadhaa barani Ulaya, zikiwamo Leipzig, Juventus, Bayern Munich, Newcastle, AC Milan, Borussia Dortmund na Atletico Madrid.

Kati ya pande hizo, ni waajiri wa zamani wa Werner ambao kwa sasa wanaongoza kinyang'anyiro cha kuwania saini yake.

Leipzig wamefanya mazungumzo na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye ana nia ya kurejea katika klabu hiyo ambayo alifunga nayo mabao 28 katika michezo 34 pekee katika msimu wake wa mwisho wa 2019/20.

RB Leipzig wameweka wazi kwa Chelsea hawataki kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ambaye ni mmoja wa mabeki wanaohitajika sana.

# Conte anataka miaka mingi Spurs



**LONDON,** England

ANTONIO Conte anataka kubakia Tottenham Hotspur kwa "miaka mingi" huku akiimarika kuifanya klabu hiyo kuwa na nguvu England na Ulaya.

Conte amekuwa na matokeo makubwa tangu alipochukua nafasi ya Nuno Espirito Santo kama kocha mkuu wa Spurs Novemba mwaka, 2021 na kuiongoza klabu hiyo kurejea katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kumaliza katika nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu England msimu uliopita.

Mtaliano huyo ameungwa mkono katika soko la usajili kabla ya msimu wa 2022-23, akiwaleta wachezaji kama Richarlison, Yves Bissouma, Ivan Perisic, Clement Lenglet na Djed Spence.

Conte yuko chini ya mkataba hadi Juni mwakani, lakini kocha huyo wa zamani wa Italia anasema anataka kubaki na klabu hiyo ya London kwa muda mrefu.

Alisema hayo kabla ya mechi ya mwisho ya Spurs ya kujiandaa na msimu dhidi ya AS Roma jana Jumamosi: "Kama nilivyosema hapo awali, mradi wetu, mpango wetu ni kujaribu kuwa washindani, zaidi ya siku zilizopita.

"Lakini unajua kabisa kwenye soka unajenga kitu muhimu ndani ya siku moja, mwezi mmoja, mwaka mmoja unatakiwa kwenda hatua kwa hatua na kujaribu kuongeza ubora, kuongeza idadi ya wachezaji kwenye kikosi chako.

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA

# MILIONI 75/- ZAKUSANYWA SULE, SHAURI WAKING'ARA

**Na Baraka Jamali,** MTWARA

WAKATI jumla ya Sh. milioni 75 zikikusanywa katika mbio za Korosho Marathon zilizofanyika jana mkoani hapa, mwanariadha, Inyasi Sule aliibuka mshindi wa kilomita 21 kwa upande wa wanaume wakati, Magdalena Shauri aling'ara kwa wanawake, wote kutoka jijini Arusha.

Sule aliibuka mshindi baada ya kutumia saa 1:01:45 wakati Magdalena yeye alitumia saa 1:25:23 na kila mmoja amepata zawadi ya Sh. milioni nane huku nafasi ya pili kwa wanaume ikichukuliwa na Shingade Giniki kutoka Manyara aliyetumia saa 1:03:08 na Francis Damian alimaliza watatu kwa kutumia saa 1:04:33.

Mshindi wa pili kwa wanawake ni Maserina Issa wa Arusha aliyetumia saa 1:28:25 na kujipatia Sh. milioni nne, Angel John aliyetumia saa 1:29:30 alipata Sh. milioni mbili baada ya kumaliza nafasi ya tatu huku nafasi ya nne ilikwenda kwa, Tunu Andrew aliyetumia saa 1:30:20.

Akizungumza katika kilele cha mbio hizo, mgeni rasmi, Zainab Telack ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Lindi, alisema mashindano ya mwaka huu yawe chachu ya kuandaa kwa ubora zaidi hapo mwakani na washiriki wawe mabalozi wazuri wa kutangaza fursa ikiwamo ya zao la korosho.

"Mashindano haya yawe chachu ya kufanya maandalizi mazuri kwa mwaka unaofuata, kila mmoja wetu awe balozi wa kutangaza fursa za utalii na zao letu la korosho kupitia mbio hizi ambazo zimefanya vyema mwaka huu.

"Niwapongeze waandaaji, washindi wa leo na wale wote ambao wameshiriki na wale waliochangia ndugu zetu wabanguaji wadogowadogo na mimi niko tayari kutoa kibali hawa wabanguaji waje kununua kurosho Lindi kwa sababu kupitia mbio hizi zitachochea zaidi maendeleo ya Lindi," alisema Telack.

Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho, Francis Alfred alisema wameamua kuanzisha mbio hizo ili kukusanya fedha za kuwasadia wajasiriamali wadogo wadogo wafanikiwe kutimiza ndoto zao.

"Tumefanikiwa kukusanya kiasi cha Sh. milioni 75 ambayo hii itakwenda kusaidia ndugu zetu wabanguaji wadogo wadogo wenye uhitaji ili kuongeza thamani ya zao la Korosho," alisema mkurugenzi huyo.

Magdalena alisema alijitahidi kupambana ili aweze kushinda zawadi hiyo ambayo alikuwa na uhitaji mkubwa wa kuichukua na anashukuru Mungu ametenda.

Naye Marco Marco ambaye aliibuka kinara katika mbio za kilomita 10 upande wa wanaume alisema amefarijika kumaliza wa kwanza katika mbio hizo na anaimani mwaka unaofuata atafanya juu chini ili kuchukua zawadi kubwa zaidi.

"Ushindi wangu ni chachu na deni kwangu kuhakikisha msimu ujao wa mashindano haya ninakuwa mshindi wa kwanza kwa mbio ndefu kilomita 21, ninaamini nitafanya hivyo" alisema Marco.




Mshindi wa kwanza wa mbio za kilomita 21 za Korosho Marathon kwa upande wa wanawake, Magdalena Shauri akiwa amembeba mtoto wake baada ya kukabidhiwa mfano wa hundi ya Sh. milioni nane ambayo ni zawadi kutokana na kushika nafasi hiyo. **PICHA: BARAKA JAMALI**

# Ilamfya asajiliwa Mtibwa Sugar

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Prisons imeendelea kuiboresha kikosi chake kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kumsajili, straika wa Dodoma Jiji, Khamisi Mcha wakati Mtibwa Sugar wakimnasa mshambuliaji wa zamani wa Simba na KMC FC, Charles Ilamfya.

Msemaji wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru aliliambia gazeti hili wanaendelea vyema na mchakato wa usajili na wataweka hadharani taarifa ya wachezaji ambao watakuwa wamemalizana nao.

Kifaru alisema wamesajili wachezaji wenye ubora na viwango ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kupambana na si kurudia kukalia kuti kavu.

"Karibuni mafundi, tunaamini ndani ya hii miaka yetu miwili kuanzia sasa mengi yataonekana juu ya uwezo wenu uwanjani," uongozi wa Prisons uliandika katika taarifa yake rasmi.

Prisons iliyonusurika kushuka daraja, inafanya mazoezi kwenye Uwanja wa Ndani ya Chuo cha Ufundi, Ruanda jijini Mbeya wakati Mtibwa Sugar pia imenasa saini ya beki wa kati, Idd Mobby kutoka Polisi Tanzania.

SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 31/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3706 | Suwon City vs Daegu | 2.32 | 3.20 | 2.81 |
| 13:30 | 5622 | Anyang vs Busan I Park | 1.66 | 3.49 | 4.72 |
| 14:00 | 1604 | Bremer SV vs Schalke 04 | 40.63 | 14.22 | 1.04 |
| 14:00 | 3963 | Sunderland vs Coventry | 2.59 | 3.24 | 2.59 |
| 14:00 | 4788 | BSV Rehden vs Sandhausen | 29.62 | 8.99 | 1.09 |
| 14:30 | 5261 | Racing Genk vs Standard Liege | 1.49 | 4.30 | 5.81 |
| 15:00 | 1330 | Aalborg vs Horsens | 1.72 | 3.66 | 4.51 |
| 15:00 | 3561 | Aarhus vs Randers | 2.54 | 3.29 | 2.64 |
| 15:00 | 4843 | Nizhny Novgorod vs CSKA Moscow | 4.10 | 3.45 | 1.83 |
| 16:00 | 1334 | Elfsborg vs BK Hacken | 2.08 | 3.74 | 2.85 |
| 16:00 | 2254 | Sirius FK vs Mjallby | 2.34 | 3.15 | 2.81 |
| 16:00 | 4829 | Hammarby vs IFK Varnamo | 1.30 | 4.92 | 7.87 |
| 16:30 | 2041 | Kaiserslautern vs SC Freiburg | 5.31 | 4.03 | 1.60 |
| 16:30 | 3389 | Blau-Weiss Lohne vs Augsburg | 21.43 | 11.23 | 1.08 |
| 16:30 | 4560 | SV Oberachern vs Monchengladbach | 35.61 | 17.30 | 1.03 |
| 16:30 | 4739 | Molde vs Stromsgodset | 1.40 | 4.92 | 6.43 |
| 16:30 | 4851 | FV Engers 07 vs Arminia Bielefeld | 20.30 | 9.34 | 1.11 |
| 16:30 | 4873 | TSV Schott Mainz vs Hannover | 45.70 | 12.19 | 1.05 |
| 16:30 | 5437 | SV Rodinghausen vs Hoffenheim | 17.27 | 8.13 | 1.14 |
| 16:30 | 5744 | Sarpsborg vs Lillestrom | 2.36 | 3.46 | 2.76 |
| 17:00 | 2514 | St Patricks vs Waterford Utd | 1.33 | 4.61 | 7.46 |
| 17:00 | 3887 | St Mirren vs Motherwell | 2.56 | 3.11 | 2.76 |
| 17:00 | 4777 | Eupen vs Brugge | 5.82 | 4.62 | 1.46 |
| 17:00 | 5093 | Viborg FF vs Copenhagen | 3.83 | 3.57 | 1.87 |
| 17:30 | 1754 | Spartak Moscow vs Gazovik Orenburg | 1.59 | 3.96 | 5.01 |
| 17:30 | 1994 | FC Winterthur vs FC Lugano | 2.45 | 3.36 | 2.71 |
| 17:30 | 3958 | BSC Young Boys vs Grasshoppers | 1.38 | 5.03 | 6.64 |
| 17:30 | 5099 | Kryliya Sovetov vs Torpedo Moscow | 1.56 | 4.01 | 5.22 |
| 18:00 | 2848 | Austria Vienna vs LASK Linz | 2.55 | 3.33 | 2.45 |
| 18:00 | 5819 | Austria Klagenfurt vs Rapid Vienna | 3.24 | 3.58 | 1.95 |
| 18:30 | 4407 | Celtic vs Aberdeen | 1.25 | 5.62 | 10.03 |
| 19:00 | 1193 | Silkeborg vs Brondby | 1.92 | 3.55 | 3.66 |
| 19:00 | 1331 | Eintracht Braunschweig vs Hertha BSC | 4.36 | 3.65 | 1.80 |
| 19:00 | 1367 | Erzgebirge Aue vs Mainz | 6.51 | 4.68 | 1.44 |
| 19:00 | 1813 | England W vs Germany W | 2.36 | 3.14 | 2.80 |
| 19:00 | 2069 | Spartak Trnava vs Sport Podbrezova | 1.47 | 4.13 | 5.70 |
| 19:30 | 2236 | RFC Seraing vs Kortrijk | 2.86 | 3.31 | 2.37 |
| 19:55 | 4887 | NK Osijek vs Slaven Belupo | 1.43 | 4.24 | 6.11 |
| 20:00 | 2572 | Sparta Prague vs Slovan Liberec | 1.39 | 4.80 | 7.56 |
| 20:00 | 2809 | Rostov vs FK Khimki | 1.81 | 3.54 | 4.09 |
| 20:00 | 4124 | Sligo Rovers vs Wexford Youths | 1.23 | 5.50 | 9.63 |
| 21:00 | 4439 | Paris St Germain vs Nantes | 1.36 | 4.87 | 6.31 |
| 21:15 | 2123 | Luka Koper vs Maribor | 2.59 | 3.37 | 2.40 |
| 21:30 | 4004 | Liptovsky Mikulas vs Ruzomberok | 3.28 | 3.38 | 2.00 |
| 21:30 | 5780 | Universitatea Craiova vs Rapid Bucuresti | 2.02 | 3.20 | 3.66 |
| 22:00 | 1601 | HNK Rijeka vs HNK Gorica | 1.84 | 3.45 | 3.74 |
| 22:00 | 2266 | Talaea El Gaish vs El Ittihad Alexandria | 2.34 | 2.92 | 3.27 |
| 22:00 | 3969 | Internacional vs Atletico Mineiro | 2.66 | 3.00 | 2.56 |
| 22:00 | 4320 | Royal Antwerp vs Zulte Waregem | 1.38 | 4.73 | 7.24 |
| 22:00 | 5831 | Kolubara vs Mladost Lucani | 2.36 | 3.14 | 2.80 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Julai 31, 2022

Nipashe




Werner akaribia kutua RB Leipzig

HABARI UK 22



Mshambuliaji wa Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars), Kibu Dennis (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa Somalia, Bile Elmi katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana. Stars ilishinda mabao 2-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Stars yatakata, Simbu ang'ara

●●● Yaifuata Uganda CHAN, Tanzania ikipata medali ya fedha katika mashindano ya...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars), ikisonga mbele katika mbio za kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) kwa kuifunga Somalia mabao 2-1, mwanariadha, Alphonce Simbu amenyakua medali ya fedha katika mbio za mashindano ya Jumuiya ya Madola zilizofanyika nchini Uingereza jana.

**Stars imeiondoa Somalia kwa ushindi wa jumla wa mabao 3-1 na sasa itakutana na Uganda mwezi ujao katika hatua inayofuata.**

Abdul Suleiman 'Sopu', kwa mara nyingine tena dakika ya 33, aliifungia Stars bao dhidi ya Somalia kama alivyofanya Jumamosi iliyopita, safari hii akifunga bao kwa shuti la chinichini alilolipiga akiwa mbali ya lango akimpita kipa, Abdulrahman Mahmoud na mpira kujaa wavuni.

Kiungo mshambuliaji huyo mpya wa Azam FC pia alisababisha goli la pili, baada ya kuingia na mpira ndani ya eneo la hatari kabla ya kufanyiwa madhambi na Ayman Mohamed na bao kuzamishwa wavuni na Dickson Job dakika ya 64.

Hadi mapumziko, Stars inayofundishwa na Kocha Mkuu, Kim Poulsen ilikuwa mbele kwa bao 1-0.

Ni mechi iliyoanza bila msisimko wowote, Stars ikijitahidi kumiliki mpira na kufanya shambulizi dhaifu, huku wachezaji wa Somalia wakicheza mchezo wa kuzuia zaidi, wakitaka kushambulia kwa kushtukiza, lakini mipira yao mirefu iliishia kwenye vichwa au miguu ya mabeki au viungo wakabaji wa Stars.

Kwenye mechi hiyo, straika George Mpole angeweza kufunga mabao matatu kipindi cha kwanza kama angekuwa makini, kwa sababu dakika ya 15 tu, alimegewa pande na Sopu, akiwa anatazamana na kipa Mahmoud, lakini shuti lake dhaifu liliokolewa na kipa huyo.

Dakika nne baadaye alipata nafasi kama ya mwanzo, lakini safari hii shuti lake liliwababatiza mabeki wa Somalia na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda na akakosa tena bao lingine dakika ya 40.

Kipindi cha pili Somalia iliingia ikiwa imebadilisha mfumo, kwani 'walifunguka' na kulishambulia lango la Stars kama nyuki na haikushangaza iliposawazisha bao dakika ya pili tu baada ya mapumziko.

Ulikuwa mpira mrefu uliopigwa kutoka katikati ya uwanja na kumkuta Farhan Ahmed ambaye aliwahadaa mabeki wa Stars kabla ya kufumua shuti kali ambalo lilimgonga kichwani beki, Bakari Mwamnyeto na kumpoteza maboya kipa Abutwalib Mshery, ukagonga mwamba wa juu na kudundia nyavuni.

Lilikuwa ni bao la kusawazisha na kuwapa wakati mgumu wachezaji wa Stars ambao walianza kupoteana na kuwafanya wachezaji wa Somalia wakiongozwa na Isse Ibrahim, Abdulhamid Osman, Anwar Sidari na wengineo kutawala katikati ya uwanja.

Bao la mkwaju wa penalti, ndilo liloonekana kuwamaliza nguvu Somalia na kuonekana wachezaji wake wamekata tamaa.

Simbu alitumia saa 2: 12: 29 wakati mshindi wa medali ya dhahabu katika mashindano ya riadha ya Jumuiya ya Madola yaliyofanyika katika mji wa Birmigham, Uingereza jana Mganda Victor Kiplangat alitumia saa 2:10: 55.

Kufuatia ushindi huo, Simbu atajinyakulia kitita cha Dola za Marekani 7,500 kutoka kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pia ikimpongeza kwa kupeperusha vyema bendera ya nchi kwenye mashindano hayo.

Pia Mtanzania mwingine, Hamisi Mesai alifanya vyema katika mashindano hayo kwa kushika nafasi ya nane baada ya kutumia saa 2:15:59.

# Simba SC, Yanga mpaka kieleweke

**Na Saada Akida**

WAKATI mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wanatarajia kucheza mchezo mwingine wa kirafiki dhidi ya Friends Rangers utakaofanyika leo, watani zao, Simba iliyoko Misri wameendelea na programu maalumu ya mazoezi kuhakikisha wanarejea nchini wakiwa 'wameiva'.

Hata hivyo kikosi cha Simba juzi kilipata mapumziko na kilitumia nafasi hiyo kutembelea meli ya kitalii ambayo ndani yake ina michezo mbalimbali.

Kuelekea mechi ya kirafiki ya leo, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi alisema amefurahi kuona nyota wake wawili wa kimataifa, Bernard Morrison na Yannick Bangala wamerejea na kujiunga rasmi na kambi hiyo iliyoko Kigamboni jijini Dar es Salaam.

Nabi alisema amewaandalia programu maalumu Morrison na Bangala ili kuhakikisha wanakuwa fiti kama wachezaji wenzao ambao walianza mazoezi mapema.

"Tayari wachezaji hao wameshafika na watakuwa na programu maalum ili kuwa fiti, tunatarajia kucheza mechi nyingine kesho (leo) ya kirafiki kwa ajili ya kupata mwanga zaidi wa kikosi changu," alisema Nabi.

Alisema alifurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na nyota wake mbalimbali akiwamo Stephane Aziz Ki katika mchezo wao wa kirafiki dhidi ya Transit Campe ambapo walipata ushindi wa mabao 5-0.

"Hizi mechi nzuri sana, bila kuangalia matokeo kikubwa unapokuwa na mechi za mazoezi ndio unatambua kama wachezaji wamekuelewa na kutakiwa kuongeza mechi nyingine ili kupata kikosi kizuri," alisema Nabi.

Mabao ya Yanga katika mchezo dhidi ya Transit Camp yalifungwa na Aziz Ki, Heritier Makambo na Fiston Mayele aliyefunga magoli matatu 'hat-trick'.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kambi yao inaendelea vyema na kila mchezaji anajituma ili kumshawishi kocha kumweka kwenye mipango yake.

"Ushindani wa namba umechangiwa na uwepo wa kocha mpya, hali hiyo inaonekana mazoezini na kwenye mechi za kirafiki tunazocheza, kikosi kimeiva, kiko moto," Ahmed alitamba.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >